**Bodaboda** zaidi ya 50 zakamatwa operesheni kamata kamata ya Polisi

UKURASA 4





**Baba** ajinyonga hadi kufa baada ya mke kumwachia watoto

UKURASA 4



Nipashe

TESA

Jumanne Agosti 10, 2021

TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI

Ukurasa 12

DC Shinyanga anapomaliza machungu walimu shuleni

Ukurasa 13

Vituo vya umahiri viing'arishe Tanzania visiishie kuwa hadithi

NIDA ni maji shingo vitambulisho vya utaifa

Ukurasa 14

ELIMU

NA MARY GEOFREY

MABINGWA AFYA WAONGEZA UHAKIKA CHANJO

■Watoa hofu kuganda damu, wasema haijaripotiwa nchini

■Washauri kuacha kunywa siku kadhaa kabla na unapochanja

WAKATI Watanzania wakiendelea kupata chanjo ya UVIKO-19 katika vituo maalumu nchini kote, wataalamu na mabingwa wa afya, wanawahimiza wananchi kuchanja na kupuuza sintofahamu kwenye jamii, ambayo inaweza kuwa chanzo cha hofu kwa baadhi ya watu.


UKURASA 11



# Nipashe

Jumanne Agosti 10, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya

ISSN 0856 • Na. 0580668

MWANGA WA JAMII

www.ippmedia.com



www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US


# Shahidi: Sabaya aliniwekea bastola kichwani, mdomoni


UKURASA 3




Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akitoa heshima za mwisho kwenye kaburi la aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Ushetu na Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Elias Kwandikwa, yaliyofanyika katika makaburi ya familia Kijiji cha Butibu Kata ya Kinamapula, Halmashauri ya Ushetu Wilaya ya Kahama mkoani Shinyanga, jana. **PICHA: SHABAN NJIA**

## YALIYOMO


UKURASA WA 4


### SABABU KUPAA MFUMUKO WA BEI HIZI

MFUMUKO wa bei wa taifa kwa mwaka ulioishia mwezi Julai, 2021 umeongezeka hadi asilimia 3.8 kutoka asilimia 3.6 kwa mwaka ulioishia mwezi Juni, 2021, huku bidhaa za vyakula, mavazi pamoja...


UKURASA WA 5


### RAIS MWINYI ATAKA TRA, ZRB KUSHIRIKIANA

RAIS wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi ametaka ushirikiano kati ya Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) pamoja na Bodi...

## ACT YATOA MASHARTI UCHAGUZI WA KONDE


UKURASA 3


# Samia afunguka kukamatwa kwa Mbowe


UKURASA 2



**MICHEZO** KISINDA APIGWA BEI, AUCHO AITULIZA YANGA UK. 24

**MAONI, KATUNI** UK.6

HABARI KITAIFA

# Samia afunguka kukamatwa kwa Mbowe

Na Elizabeth Zaya

RAIS Samia Suluhu Hassan amesema kesi inayomkabili Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Freeman Mbowe, ni ya kuachia Mahakama pekee ndiyo iamue.

Rais Samia alitoa kauli hiyo jana wakati akihojiwa na kituo cha Televisheni cha BBC.

"Mimi sidhani kama kesi inayomkabili Mbowe imechochewa kisiasa, kwa sababu ninavyojua, Mbowe na wenziwe walifunguliwa kesi mwezi wa tisa mwaka jana, nadhani wenzie kesi zao zimesikilizwa, yeye uchunguzi ulikuwa unaendelea, nadhani sasa hivi polisi ndio wamekamilisha wakaona waendelee," alisema Rais Samia.

"Na ukumbuke kwamba Mbowe hakuwapo nchini na alivyoingia tu nchini akaanzisha hayo maandamano ya kudai Katiba mpya. Nadhani ilikuwa ni 'calculation' kwamba akikamatwa ionekane ni njama za kisiasa. Nadhani kwa sababu kesi iko mahakamani, ni vema tuiachie mahakama ionyeshe dunia kwamba tuhuma hizo ni za kweli au siyo za kweli," alisema Rais Samia.

**UHURU WA DEMOKRASIA**

Alipoulizwa endapo Tanzania inao uhuru wa demokrasia ya siasa, Rais Samia alisema uhuru huo upo na akatofautisha kati ya uhuru huo wa demokrasia na fujo za demokrasia ya kisiasa.

"Demokrasia ya kisiasa ipo, na hapa naomba nitofautishe kati ya demokrasia ya kisiasa na fujo za kisiasa. Demokrasia ya kisiasa ndiyo hiyo tuna vyama vya siasa, wana vyombo vyao, wanajadili mambo yao. Kwa mfano tuna Baraza la Vyama vya Siasa, huko wanajichagua wenyewe, wanajadili mambo yao ya kisiasa, wanaelewana huko," alisema Rais Samia.

"Kuna kamati za vyama vyenye wabunge bungeni, na wenyewe wana ya kwao, wanakaa wanazungumza, wanajadiliana huko. Lakini kuna vyama vyenyewe vya siasa ambavyo vimeundwa na katiba zao na kwenda kwao au kufanya kazi kwao kunategemea katiba zao hizo."

"Kwa mfano, chama changu cha Mapinduzi, Katiba yangu labda inaniambia kwamba katika mwaka nitakuwa na vikao viwili vya Halmashauri Kuu ya chama, labda vikao sita vya Kamati Kuu, na vikao vingine katika ngazi za chini, mikoa na wilaya, na hivyo vimeelezewa kwamba wajumbe ni nani na kila kitu.

Hivyo vikao vinaendeshwa bila bughudha na bila kuomba kibali polisi. Kwa sababu katiba imeshaelezwa, imepita kote na inajulikana."

"Na vivyo hivyo, vyama vingine vyote, vina katiba zao zina na system (mifumo) yao ya mikutano, wajumbe wao ni kina nani, hivyo wako free (huru) kufanya wakati wowote. Kitu ambacho hakipendezi ni kutaka uhuru wa kufanya fujo za kisiasa.

Labda tumemaliza uchaguzi, serikali imeundwa, kinachotakiwa kuendelea ni kujenga nchi, uwe una chama gani wote mnakuja pamoja mnajenga nchi yenu, lakini inatokea chama ambacho wao wanataka tu kuitisha maandamano kila siku, maandamano yasiyo na mwisho, labda sijui mkutano uko, vurugu za hapana na pale, hapana."

**UHURU WA VYOMBO VYA HABARI**

Rais Samia alisema uhuru wa kujieleza kwa vyombo vya habari uliopo ni mkubwa na kwamba kama kiongozi wakati mwingine wanafanya hivyo ili watu kutoa yaliyopo moyoni ili yafanyiwe kazi.

"Hakuna chombo kinacholalamika, kuna uhuru wa kutosha wanajieleza na tena mpaka wanavuka mipaka saa nyingine, lakini kama kiongozi unavaa ngozi ngumu. Lakini wakati mwingine kusema kwao, bora umpe mtu kutoa alichonacho, umsikie ili kama kiongozi useme ahaa kumbe kuna hiki kinalalamikiwa basi unakifanyia kazi," alisema Rais Samia.

"Kuliko kuwabana hawasemi. Hujui wanafukuta na nini ndani, sasa Tanzania kuna uhuru wa kutosha, vyombo vyote vya habari viko huru, anayefuata sheria na anayefuata maadili ya kazi zao, wapo wanafanya kazi zao.

**KUKUTANA NA VYAMA VYA SIASA**

Rais Samia alisema yupo tayari kukutana na kufanya mazungumzo na vyama hivyo wakati wowote.

"Niseme tu kwamba nitakutana nao. Sikutaka nikutane nao wakiwa wamenyambuka nyambuka, kama tayari wamejiunda na kamati zao ndogondogo, tutatafuta siku tuzungumze nao.

Na mimi nataka nikutane nao, niwaambie kwamba tumemaliza uchaguzi, sasa tukajenge nchi. Na mimi nimesema Watanzania wote watajenga nchi na si chama kimoja tu, mimi mtu yeyote anayeweza kufanya vizuri namchukua tu," alisema Rais Samia.



Rais Samia Suluhu Hassan akihojiwa na Mtangazaji wa Kituo cha Televisheni cha BBC, Salim Kikeke, jana. **PICHA: BBC.**

# Majaliwa: Serikali itaenzi aliyoyaacha Kwandikwa

**Na Neema Sawaka,** USHETU

WAZIRI Mkuu Kassim Majaliwa, ameongoza waombolezaji katika maziko ya aliyekuwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Elias Kwandikwa, katika Kijiji cha Butibu, Kata ya Kinamapula Halmashauri ya Ushetu, wilayani Kahama mkoani Shinyanga.

Maziko hayo yalifanyika jana nyumbani kwa marehemu Kwandikwa na kuhudhuriwa na viongozi wa chama na serikali kutoka mikoa mbalimbali hapa nchini.

Kabla ya maziko, Askofu wa Kanisa Katoliki Jimbo Kuu la Kahama, Ludovic Minde, aliongoza ibada fupi na waombolezaji walishiriki kumsindikiza marehemu katika nyumba yake ya milele kijijini hapo.

Majaliwa aliongoza waombolezaji hao kwa niaba ya Rais Samia Suluhu Hassan.

"Sisi kama serikali tutaenzi mipango yake mizuri aliyoiacha na niahidi serikali itatekeleza miradi yote na madiwani wasimamie miradi yote vizuri kwa kuenzi aliyoyafanya na wabunge wa Mkoa wa Shinyanga poleni mlikuwa na mshikamano Mungu awape nguvu pamoja na familia yake," alisema.

Waziri Majaliwa alisema marehemu alikuwa mtu shupavu ambaye alitumikia taifa kwa uaminifu na kwamba wasifu wake uliosomwa ulidhihirisha hilo.

Kwa upande wake, akitoa mahubiri katika ibada hiyo, Askofu Minde, alisema kuwa maandiko yanasema vitu vyote vipo kwa ajili yake Mungu na mipango yake ipo kamili hivyo mafundisho yanasema anayekufa bado watu wanampenda atakwenda kustarehe.

Alisema wakati wa uhai wake marehemu alisaidia shughuli za kiuchungaji na hakubagua eneo lolote na kwamba alikuwa tayari kutoa ushauri.

"Tunapomsindikiza katika makao yake ya milele kweli tulimpenda na alikuwa mtu wa Mungu aliyevaa hofu ya Mungu na kupenda maendeleo kwani hata upande wa kanisa alituleleza tuthubutu na tulipenda aendelee kuwapo ila Mungu alimpenda zaidi," alisema askofu Minde.

Pia, salamu mbalimbali zilizotolewa na wawakilishi akiwamo Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Daniel Chongolo.

Chongolo alisema chama kimempoteza mtu aliyekuwa msaada na kukipenda chama hivyo naomba Mungu ampumzishe kwa amani.

Akitoa salamu katika maziko hayo, Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi, Jenerali Venance Mabeyo, alisema marehemu alikuwa mtu wa kujitoa na kiongozi bora.

Marehemu Kwandikwa alizaliwa mwaka 1966 na katika uhai wake alitumikia nafasi mbalimbali za uongozi ikiwamo Mbunge wa Jimbo la Ushetu, mkoani Shinyanga, Naibu Waziri wa Ujenzi na Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

Kwa upande wake, Waziri wa Mambo ya Ndani, George Simbachawene, akitoa salamu kwa niaba ya mawaziri alisema marehemu alikuwa mchapakazi na mwenye uhusiano mzuri na jamii.

Marehemu alizikwa jana kwa heshima zote na kupigiwa mizinga 17 kwa mujibu wa taratibu za kijeshi.

Waombolezaji wameambiwa kuwa marehemu alianza kuugua Julai 15 na kulazwa Hospitali ya Jeshi ya Lugalo kabla ya kuzidiwa na kuhamishiwa Hospitali ya Taifa ya Muhimbili na alifariki Agosti 2, mwaka huu.

## HABARI KITAIFA

# Shahidi adai Sabaya kumwekea bastola kichwani

**Na Allan Isack,** ARUSHA

SHAHIDI wa nane wa Jamhuri, Magdalena Mallya au Zulpha (32) ambaye ni mke wa Bakari Msangi aliyekuwa shahidi wa sita katika kesi ya jinai inayomkabili aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai, mkoani Kilimanjaro, Lengai Ole Sabaya(34), amekamilisha ushahidi wake kwa kudai Sabaya alimwekea bastola kichwani na mdomoni akitishia kumuua.

Washtakiwa wengine wawili katika shauri hilo ni Sylvester Nyegu (26) na Daniel Mbura (38).

Akihojiwa na wakili wa upande wa utetezi, Dancan Oola, shahidi huyo alidai Sabaya alimshikia bastola huku akimweleza kwamba atamwaga ubongo.

Alidai baada ya kumtafuta kwa muda mrefu mume wake alimpigia akimweleza kwamba yupo Tulia Lodge ameshikiliwa na kutekwa na Sabaya.

"Kuna utofauti kati ya kushikiliwa na kutekwa na Msangi, baada ya kufanyiwa matendo yote ya kiuhalifu aliachiwa nikiwa naye," alidai shahidi huyo.

Magdalena, aliieleza mahakama hiyo kuwa hakushuhudia Sabaya akimpiga mume wake kwa kuwa hakuwa katika eneo la duka la Mohamed Saad.

Naye wakili mwingine wa utetezi, Moses Mahuna, alimuhoji shahidi huyo kama ifuatavyo:

Wakili: Mume wako alikwambia kuwa ameshikiliwa au ametekwa na Sabaya.

Shahidi: Msangi alinieleza kuwa alitekwa nyara na kutishiwa kuuawa na Sabaya na walinzi wake.

Nikiwa katika lango la kuingilia la Tulia Lodge, nilimpigia magoti huku nikiwa nimenyoosha mikono juu, nikimwomba Sabaya kumuachia Msangi, kwa kuwa alikuwa amemteka nyara na kumweka kwenye gari lake.

Nilimuomba Sabaya asimuue mume wangu kwa kuwa yupo kwenye gari lake nilimwelekeza kuwa mimi na mtoto wangu ni wagonjwa sana na tunamtegemea, nikiwa nalia gari lilisimama mbele yangu, wakashuka vijana wawili wakiwa bunduki mmoja alinipiga nayo mgongoni nilipata maumivu makali nikawa nimeanguka chini, waliniambia nisogee njia nilipata maumivu makali kwa kuwa siku si nyingi nilikuwa nimefanyiwa opereshini ya uzazi.

Shahidi huyo alidai kuwa aliendelea kulia na kumwomba amwachie mume wake huku vijana wawili wakimshika bega la kushoto na kulia na kumburuza kumtoa njiani.

Alidai kuwa walimsogeza karibu na gari la Sabaya na alifungua kioo. "Nilivyomuona nilimwomba asimuue mume wangu nilimweleza hata kama kuna kosa amelifanya wampeleke kituo cha polisi, alichonijibu aliniambia kuwa nifunge mdomo."

"Sabaya aliniambia kwa hasira funga mdomo wako, huku akigeuka nyuma kwenye siti za gari lake, ghafla mlango wa gari wa nyuma ulifunguliwa wakamshusha Msangi, kwenye gari akiwa mwenye majeraha mekundu sana ya kuivia damu, sikio lake moja lilikuwa likionyesha kwamba lilikuwa likidondosha damu na wakati huo ilikuwa imeshaganda, alikuwa na mwonekano wa mtu asiyekuwa na nguvu."

Pia, alidai baada ya Msangi kushushwa kwenye gari, Sabaya aliagiza wasindikizwe hadi kwenye gari lake, wakazungumze huku wakiwa chini ya ulinzi.

"Tulipoingia ndani ya gari, Msangi alifungua zipu ya suruali yake na alitoa simu zake mbili na kunipatia, aliniambia kwamba anahisi maumivu makali ya kichwa, niliwasha simu yangu kumuangalia alikuwa na majeraha ya kupigwa hadi damu imeivia sehemu za shingoni, usoni, mashavuni na masikioni."

Aliendelea kudai mahakamani hapo kuwa wakati akikumwomba amsamehe mume wake, Sabaya alitoa bastola na kumwekea kichwani upande wa kushoto karibu na sikio huku akimtukana matusi ya nguoni.

"Niliendelea kumwomba, lakini alihamisha bastola kutoka kichwani na kuniwekea mdomoni huku akinitusi matusi ya nguoni akidai kwamba mimi nalilia mapenzi wakati wanawake wengine wanalilia fedha, wakati huo akiwa mwenye jazba na hasira sana aliniambia atanimwaga ubongo kwa kunipiga risasi."

Shahidi huyo alidai baada ya kutishiwa alinyamaza na Sabaya akimweleza maisha ya mume wake yapo mikononi mwake na yote hayo yasingetokea kwa sababu ya kiherehere chake kimemponza.

Aliendelea kudai kuwa Sabaya alimwambia mume wake akikubali kutoa ushirikiano wa kile anachokihitaji wataelewana na asipotoa ushirikiano wasilaumiane.

Pia, alidai Sabaya aliwaagiza walinzi wake kumtoa kwenye gari lake kwa kumburuza hadi kwenye gari lake na kuondoka huku wakimuacha akiwa amekaa chini.

"Tulipotoka hapo hadi mataa ya Triple A, barabara ya kuelekea Ngarenaro, tukiwa kwenye gari jirani yangu aliniambia kuna magari yanatufuatilia kwa kuwa yalikuwa yanatupigia honi, yalikuwa ni magari ya Sabaya na vijana wake."

Alidai magari hayo yalikuwa kwenye mwendo wa kasi yakiwafukuza na kuwapita na kuwazuia kwa mbele na ghafla kijana mmoja alishuka na kwenda kumgongea kwenye gari lake. Aliposhusha kioo cha gari alimwambia kwamba Sabaya anamuhitaji.

"Sabaya aliniuliza jina langu, nilimweleza kuwa naitwa Zulpha, aliniuliza tena kama ninamfahamu Mohamed Saad, nilimjibu hapana simfahamu," alidai.

Pia shahidi huyo, aliieleza mahakama hiyo kuwa Sabaya alimuhoji ni kwa nini hamfahamu rafiki ya mume wake, naye alimjibu kwamba hamfahamu mtu huyo.

"Aliniagiza niwapatie namba zangu za simu, huku akitoa agizo kuwa siku inayofuata atanipigia simu na atanielekeza wapi atakapokuwa, hivyo nimbembeleze Msangi, kwa kuwa anafahamu sehemu Mohamed Saad, alipokuwa ili tuambatane naye kumpeleka kwa Sabaya."

# ACT yatoa masharti uchaguzi mdogo Konde

**Na Mwandishi Wetu,** PEMBA

CHAMA cha ACT-Wazalendo kimesema hakitashiriki uchaguzi mdogo wa Jimbo la Konde hadi watumishi wa Tume ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC), waliohusika katika uchaguzi uliopita watakapowajibishwa.

Akisoma maazimio ya chama katika eneo la Konde Pemba wakati wa ziara maalum ya viongozi wa ACT-Wazalendo, Kiongozi Mkuu wa chama hicho, Zitto Kabwe alisema chama hicho hakitashiriki uchaguzi huo hadi watumishi wa ZEC wawajibishwe.

Zitto alisema kuwa wananchi ambao waliumizwa na kuteswa kwenye uchaguzi walipwe fidia, ili wapate haki yao.

Alisema azimio lingine ni pamoja wa kuundwa kwa kamati ya kisheria ya kuratibu maridhiano ya kijamiii, ili ZEC ionyeshe mwelekeo nini kifanyike yazidi kukua.

Aidha, azimio la tatu ni kuitaka Serikali ya Zanzibar na ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuzifanyia marekebisho sheria zote za uchaguzi kabla ya mwaka 2025, ili uchaguzi mkuu ujao uwe sawa katika kushindania nafasi za uongozi.

Alisema halitakuwa jambo la busara kila baada ya uchaguzi kuirudisha Zanzibar nyuma kimaendeleo, ni vyema umoja na maridhiano ya kisiasa kudumu muda wote.

Mjumbe wa Kamati Kuu ya chama hicho ambaye ni Makamu wa Kwanza wa Rais Zanzibar, Othman Masoud Othman, alisema kilichomfanya mbunge mteule wa Konde kutoka CCM kuachia ngazi ni mazungumzo.

Alisema vilelezo na ushahidi waliowasilisha ni matunda na matokeo chanya yaliyopatikana ya kujiuzulu kwa mbuge mteule wa jimbo hilo.

Makamu Mwenyekiti wa ACT-Wazalendo, Juma Duni Haji, alisema hawako tayari kuingia kwenye uchaguzi wakati walioharibu uchaguzi huo hawajachukuliwa hatua zozote.


The Guardian Limited

VACANCY

**Freelance Sales Executives**

**The Guardian Limited** is looking for self driven sales personnel to join our **advertising** Sales Team in **Dar es Salaam, Dodoma, Arusha, Zanzibar, Tanga, Morogoro and Kilimanjaro.**

**Responsibilities**

- Be responsible for aggressive development of new clients and growing existing business.
- Proactively develop new business avenues
- Devise and monitor business plans to ensure substantive sales
- Develop strategic solutions that meet the unique needs of each client

**Qualifications**

- The position requires someone who can deliver the set targets within deadlines under competitive working environment.
- Applicants need to be highly organized, self-motivated with a positive attitude, and can thrive on setting and reaching new goals.
- Holders of a University degree or Diploma in Business Administration
- Experience in Sales and Marketing is an added advantage

**NOTE: This is a commission Based Position**

**Please send your application via Email to vacancy@guardian.co.tz before 15th August, 2021.**

61637602

# Ajinyonga kisa mke kumwachia familia

**Na Jaliwason Jasson,** MBULU

MKAZI wa Kijiji cha Ng'wandakw Kata ya Haydom wilayani Mbulu mkoani Manyara, Philemon Tandu (50), amefariki dunia kwa kujinyonga, baada ya kuachwa na mke akiwa na watoto watano.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Manyara, Marrison Mwakyoma, akizungumza na Nipashe jana, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo.

Kamanda Mwakyoma alisema Tandu alijinyonga kwa kutumia kamba ya katani shingoni baada ya mkewe, Christina Elia (45), kumuacha akiwa na watoto watano.

Alisema chanzo cha kifo hicho ni matatizo ya familia ambapo baada ya Tandu kuachwa na mkewe alichukua uamuzi wa kujinyonga kwa kutumia kamba ya katani. Alisema baada ya mwanamke huyo kutaka kumwacha mumewe walijaribu kusuluhisha ugomvi wao ili wasiachane na walee watoto wao ila ikashindikana mwanamke huyo akaondoka.

"Tandu alijinyonga kwa kutumia kamba ya katani karibu na nyumba yake baada ya mkewe kuondoka nyumbani kwao akidai hamtaki tena na kumwachia watoto watano," alisema kamanda Mwakyoma.

Alisema baada ya majirani kuona mwili wa marehemu huyo umening'inia chini ya mti walitoa taarifa kwa askari wa kituo cha polisi Haydom ambao walipofika eneo hilo walikuta ameshafariki.

Kamanda Mwakyoma alitoa wito kwa jamii ya eneo hilo kutoshiriki matukio kama hayo kwani endapo kuna tatizo wanapaswa kukaa kama familia na kutatua kuliko kujidhuru nafsi yake mwenyewe.

Hata hivyo baadhi ya wakazi wa kijiji hicho cha Ng'wandakw walisikitishwa na tukio hilo la Tandu kujinyonga sababu ya kuachwa na mke wake na kucha watoto wao watano yatima.

Akizungumza na Nipashe, mkazi wa eneo hilo, John Thomas, alisema watoto hao wameachwa na baba yao ambaye amejiua kwa sababu ya kuachwa na mke wake bila kufahamu kuwa ndiyo anaongeza tatizo.



Naibu Waziri wa Madini, Prof. Shukrani Manya, akitoa ufafanuzi kwa waandishi wa habari mkoani Mtwara, kabla ya kuanza kwa ziara yake ya siku mbili iliyolenga kutambua changamoto zinazowakabili wachimbaji wadogo wa madini. **PICHA: ABDALLAH KHAMISI**

# Sababu kupaa mfumuko wa bei hizi

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MFUMUKO wa bei wa taifa kwa mwaka ulioishia mwezi Julai, 2021 umeongezeka hadi asilimia 3.8 kutoka asilimia 3.6 kwa mwaka ulioishia mwezi Juni, 2021, huku bidhaa za vyakula, mavazi pamoja na pango la nyumba vikitajwa kuchangia hali hiyo.

Kaimu Mkurugenzi wa Sensa za Watu na Takwimu za Jamii Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS), Ruth Minja, alibainisha hayo jana jijini Dodoma alipokuwa akitoa hali ya mfumuko wa bei wa taifa kwa waandishi wa habari.

Alisema mfumuko wa bei wa taifa ulioishia mwezi Julai 2021, umeongezeka hadi kufikia asilimia 3.8 kutoka asilimia 3.6.

"Hii inamaanisha kuwa kasi ya mabadiliko ya bei za bidhaa na huduma kwa mwaka ulioishia mwezi Julai, 2021 imeongezeka ikilinganishwa na kasi iliyokuwapo kwa mwaka ulioishia mwezi Juni 202," alisema Minja.

Aidha, alisema kuongezeka kwa mfumko wa bei kwa mwaka ulioishia mwezi Julia 2021, kumechangiwa na kuongezeka kwa mfumko wa bei wa baadhi ya bidhaa za vyakula na bidhaa zisizokuwa za vyakula.

Alisema baadhi ya bidhaa za vyakula zilizochangia kuongezeka kwa mfumko wa bei ni pamoja na ngano, kwa asilimia 6.5, unga wa ngano asilimia 6.1, nyama kwa asilimia 3.7, viazi mviringo kwa asilimia 7.9, viazi vitamu kwa asilimia 8.4 na mihogo mibichi kwa asilimia 6.4," alisema. Pia, alisema kwa upande wa baadhi ya bidhaa zisizo za vyakula zilizochangia kuongezeka kwa mfumko wa bei ni pamoja na nguo za wanawake kwa asilimia 6.4, viatu vya wanaume kwa asimia 7.1, viatu vya watoto kwa asilimia 6.4 na kodi ya pango kwa asilimia 4.9.

"Mfumko wa bei kwa bidhaa za vyakula na vinywaji baridi kwa mwaka ulioishia mwezi Julai 2021, umeongezeka hadi asilimia 5.1 kutoka asilimia 4.7 kwa mwaka ulioishia mwezi Juni 2021," alisema Minja.

Akizungumzia mfumko wa bei kwa baadhi ya nchi za Afrika Mashariki kwa mwaka ulioishia mwezi Julai 2021, alisema Kenya mfumko wa bei kwa mwaka ulioishia mwezi Julai 2021, umeongezeka hadi asilimia 6.44 kutoka asilimia 6.32 kwa mwaka unaoishia mwezi Juni 2021.

Kadhalika, Uganda mfumko wa bei kwa mwaka ulioishia mwezi Julai 2021, umeongezeka hadi asilimia 2.1 kutoka asilimia 2.0 kwa mwaka ulioishia Juni 2021.

## Operesheni ya polisi yanasa bodaboda

**Na Mwandishi Wetu,** MWANZA

JESHI la Polisi mkoani Mwanza jana limeendesha msako maalum wa kukamata pikipiki za kubeba abiria katikati ya Jiji la Mwanza.

Hata hivyo, msako huo umelalamikiwa na waendesha pikipiki hao kwa madai kwamba walikamatwa na vyombo vyao kuzuiliwa kituo kikuu cha polisi cha Nyamagana bila kuambiwa makosa yao.

Akizungumza na Nipashe muda mfupi baada ya madereva hao kukamatwa, kiongozi wa nidhamu wa waendesha bodaboda mkoani Mwanza, Emanuel Benjamin, alisema operesheni hiyo ilianza jana majira ya saa mbili asubuhi.

Alisema katika msako huo zaidi ya pikipiki 50 zilikamatwa katika eneo la katikati ya jiji, mzunguko wa samaki na mzunguko wa saa na hadi jana mchana hawakuambiwa makosa yao.

Benjamini alisema: "Ukamataji wa aina hii unatengeneza mazingira ya kuibiwa pikipiki, polisi wanapokuja kumkamata mtu halafu hawajavaa sare inakuwa ngumu kuwatambua na bahati mbaya hawasemi kosa."

Alisema matukio ya watu wasiovalia sare kukamata bodaboda yamewahi kusababisha wizi wa vyombo hivyo katika maeneo mbalimbali hususani ya pembezoni mwa Jiji.

"Pia changamoto imekuja baada ya ugonjwa wa corona, tunajua ugonjwa huu unavyoenea, unapombeba abiria kwenye pikipiki akavaa kofia ukija kumbeba mwingine anakataa, hauwezi kumwambia kila unayembeba ukafue hiyo kofia," aliongeza.

Akizungumza na Nipashe, mmoja wa madereva hao, Zakimu Vedasto, alisema alikamatwa majira ya saa 2: 15 asubuhi ya jana katika mzunguko uliopo karibu na Jeshi la Polisi kwa kosa la abiria kutokuvaa kofia.

Alisema hadi ilipofika saa tano asubuhi alikuwa hajafahamu hatima yake kwa kuwa jioni alitakiwa kupeleka hesabu kwa tajiri yake.

Vedasto alisema: "Sisi tutasimama hapa nje hadi kieleweke, tuijue hatima yetu hatuwezi kwenda nyumbani wakati hatujafanya kazi na tunategemewa na familia."

Dereva mwingine wa bodaboda, Joseph Jonas, alisema alikamatwa wakati anaenda kutoa fedha benki.

"Mimi nilikuwa naenda kutoa hela ATM, wakati naingia askari akataka funguo wa pikipiki yangu, nikakataa lakini yeye akaisukuma na kuondoka nayo na pia askari wa pale benki walimuunga mkono akataka nimpe funguo ila mimi nikakataa na ninayo hapa," alisema Joseph.

Nipashe lilimtafuta Kamanda wa Polisi mkoani Mwanza, Ramadhan Ng'anzi, kupata undani wa operesheni hiyo kamata bodaboda, ambaye alikiri kuwapo kwa msako huo, kwamba waendesha bodaboda hao wataruhusiwa kuchukua vyombo vyao ingawa hakusema ni lini.

# Kesi ya Kikatiba ya Mbowe kusikilizwa

**Na Kulwa Mzee**

MAHAKAMA Kuu Kanda ya Dar es Salaam imekubali maombi ya Mwenyekiti wa CHADEMA, Freeman Mbowe, kupitia Wakili Peter Kibatala kuwasilisha kiapo cha nyongeza katika kesi ya Kikatiba ya kupinga ukiukwaji wa haki zake za kikatiba na mteja wake kuhudhuria katika shauri hilo.

Uamuzi huo wa jopo la majaji watatu ulitolewa jana, wakati kesi hiyo ilipoitwa, kwa ajili ya kutajwa.

Wakili Kibatala aliomba kuwasilisha kiapo cha nyongeza, ili kuweka nyongeza ya mambo mbalimbali na Mahakama ilikubali afanye hivyo, hadi kufikia Agosti 15, mwaka huu.

Jopo la Majaji watatu, Jaji John Mgeta, Jaji Steven Magoiga na Jaji Leila Mgonya wanaosikiliza shauri hilo waliamuru upande wa Jamhuri kujibu kiapo kinzani ndani ya siku 14 na Mahakama itapanga tarehe ya kuanza kusikiliza Agosti 30, mwaka huu.

Pia, Wakili Peter Kibatala aliomba mahakama itoe hati ya kumleta Mbowe kila kesi hiyo inaposikilizwa, Mahakama ilikubali ombi hilo na kutoa hati, mshtakiwa huyo ataletwa Agosti 30, mwaka huu.

Upande wa mlalamikaji unawakilishwa na Kibatala, Wakili John Mallya na Frederick Kihwelo huku Jamhuri ikiwakilishwa na Wakili Pius Hillar, Christopher Msigwa na Wakili Hang Changa.

Agosti 2, mwaka huu, Mbowe kupitia Wakili wake, Peter Kibatala aliwasilisha maombi Mahakama Kuu akitaka itamke, kwamba kuna ukiukwaji wa haki zake za kikatiba katika kesi ya ugaidi inayomkabili.

Mbowe kafungua maombi dhidi ya Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP), Inspekta Jenerali wa Polisi (IGP) na Mwanasheria Mkuu wa Serikali akidai wamevunja haki zake kikatiba kwa kusindwa kumpa nafasi ya kusikilizwa kikamilifu. Katika maombi yake analalamikia kuvunjwa kwa Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai na Sheria ya Uhujumu uchumi, ambayo ameshtakiwa nayo kwa makosa ya ugaidi.

Wakili Kibatala anadai kwa mujibu wa sheria hizo mtuhumiwa anataka asishikiliwe zaidi ya saa 48, Kituo cha Polisi na akifikishwa mahakamani, Hakimu anatakiwa kuhakikisha kaelewa mashtaka yanayomkabili.

Anadai Mbowe kashikiliwa Oystebay tangu Julai 21 mwaka huu hadi Julai, alipofikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu na kushtakiwa kwa ugaidi.

Katika maombi hayo anadai sheria zimevunjwa, mteja wake alikaa kituoni zaidi ya saa 48, alilazwa sakafuni, bila kujali usalama wa afya yake, wamevunja haki zake za kikatiba,, wamemtesa na kumdhalilisha.

Polisi wanadaiwa kuvunja haki hizo kwa kushindwa kumpa nafasi ya kumsikiliza kikamilifu, walishindwa kutoa taarifa kwa mawakili wake ama ndugu yake wa karibu.

Anadai Mbowe alipelekwa mahakamani mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Thomas Simba bila kuambiwa anakwenda wapi na alipopanda kizimbani Mahakama ilikiuka haki za kikatiba kwa kushindwa kumuuliza kama kaelewa mashtaka yanayomkabili.

"Alitakiwa afahamishwe mashtaka yake kiufasaha, mashtaka mazito, mahakama haijamuuliza kaelewa ama la zaidi ya kumwambia haina mamlaka ya kusikiliza shauri hilo,"alidai Kibatala katika maombi yake.

Anadai Mbowe hakupewa hati ya mashtaka hadi Julai 27, mwaka huu mawakili wake walipokwenda nayo gerezani.

"Tunaomba Mahakama itamke kuna mapungufu na haki za Mbowe zimekiukwa," alidai Kibatala.



Wanachama wa kikundi cha wakulima kiitwacho Angaza cha Kijiji cha Buraga, Jimbo la Musoma Vijijini mkoani Mara, kinachojishughulisha na kilimo cha matikiti maji, matango na mboga, wakiandaa shamba kwa ajili ya kupanda mazao hayo juzi. **PICHA: MPIGAPICHA W3ETU**

# Rais Mwinyi ataka TRA na ZRB kushirikiana

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi ametaka ushirikiano kati ya Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) pamoja na Bodi ya Mapato Zanzibar (ZRB) ili kukusanya kodi ipasavyo.

Rais Dk. Mwinyi aliyasema hayo jana Ikulu Zanzibar wakati alipokutana na kufanya mazungumzo na Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Alphayo Japan Kidata, akiwa na ujumbe wake wakati walipofika Ikulu kwa ajili ya kujitambulisha kwa Rais.

Rais Dk. Mwinyi alisema kuwa kuna haja TRA na Bodi ya Mapato Zanzibar (ZRB) kufanya kazi kwa pamoja na azma ya kuimarisha ukusanyaji wa kodi.

Alisema ushirikiano wa pamoja kati ya taasisi hizo mbili utaondoa changamoto zilizokuwapo siku za nyuma kwa ukusanyaji wa kodi upande wa Zanzibar kutofanyika vyema.

Alisema kufanya kazi kwa pamoja kati ya taasisi hizo mbili kutasaidia kwa kiasi kikubwa kufikia lengo lililokusudiwa na kuondoa upotezaji wa kodi na kutokuwa kikwazo katika upataji wa kodi.

Aliipongeza TRA kwa juhudi zake za ukusanyaji kodi hapa nchini na kwamba hata kwa upande wa Zanzibar ufanisi umekuwa mkubwa.

Alisisitiza ni vyema mafanikio yaliyopatikana Tanzania Bara kupitia TRA yakafanywa pia kwa upande wa Zanzibar ili ZRB, iweze kufanya kazi zake ipasavyo.

Alisema Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itatoa kila aina ya ushirikiano kwa TRA kuhakikisha mafanikio yanapatikana katika ukusanyaji kodi na kuahidi kwa upande wake milango yake iko wazi kuhakikisha mafanikio yanapatikana.

Naye Kamishna Mkuu wa TRA, Alphayo Kidata, alimhakikishia Rais Dk. Mwinyi kwamba taasisi yake imekuwa na ushirikiano mkubwa kati yake na ZRB na inaendelea kufanya kazi kwa pamoja ili kuhakikisha ndoto za viongozi wakuu zinafikiwa.

Alisema TRA, imeweka mikakati kabambe kuhakikisha uwezo na uweledi uliopo katika Taasisi hiyo kwa upande wa Tanzania Bara pia, unafanya kazi kwa upande wa Zanzibar ili kuweza kufikia malengo yaliokusudiwa.

# Waziri aamuru kuondolewa K/Meneja ununuzi mbolea

**Na Beatrice Moses**

WAZIRI wa Kilimo, Prof. Adolf Mkenda, ameamuru Kaimu Meneja wa Kitengo cha Ununuzi wa Mbolea kwa Pamoja (BPS), kilichoko katika Mamlaka ya Mbolea Tanzania (TFRA), Nganga Nkonya kuondolewa kwenye nafasi hiyo, akitajwa kuhujumu juhudi za serikali za kukuza kilimo chenye tija.

Prof. Mkenda aliamuru Nganga arejeshwe wizarani ili apangiwe majukumu mengine, baada ya kubainika kuhujumu utendaji katika mfumo wa BPS na kukwamisha juhudi za serikali za kuhakikisha uingizaji wa mbolea nyingi nchini ili kuwezesha upatikanaji wake kuwa wa bei nafuu kwa wakulima.

Alitoa agizo hilo jana wakati akizungumza kwenye mkutano wa wafanyabiashara wa mbolea uliofanyika jijini Dar es Salaam, pia Naibu Waziri wa Kilimo, Hussen Bashe alihudhuria, walijadili mambo kadhaa ikiwamo kufanikisha upatikanaji wa mbolea kwa wingi.

Alisema mtumishi ameshindwa kutekeleza majukumu yake ipasavyo kwa mujibu wa matakwa ya serikali ya kuhakikisha wakulima wanapata mbolea kwa bei nafuu na kwa wakati.

"Suala la mbolea ni la kufa na kupona sio suala la mzaha huyu alikuwa anachezea mfumo huo, watu wanahitaji 'control number' yeye anawazungusha, namba ya simu ya watu kupata maelezo ya kina au msaada ikawekwa na mtu asiyejulikana na wizara, sijui ni mkulima au mfugaji yupo huko Shinyanga," alisema.

"Jambo hilo lilisababisha usumbufu kwa wafanyabiashara wenye nia njema kuleta mbolea kukosa maelekezo sahihi, hivyo kuchelewesha upatikanaji wa mbolea kwa wingi na kwa wakati," alisema Profesa Mkenda.

Aliwaeleza wafanyabiashara kuwa serikali inaendelea kufanya mapitio ya mfumo huo, imefanyia kazi maoni kadhaa yaliyotolewa na wadau wa mbolea ikiwa ni juhudi zake za kuhakikisha kilimo cha tija kinafanikiwa na kusaidia kuleta maendeleo kwa wakulima na nchi kwa ujumla.

Miongoni mwa mambo waliyoshughulikiwa ni pamoja na nchini kuboresha upatikanaji wa vibali vya kuingiza mbolea nchini (Export Permit) sasa vitatolewa kwa njia ya mtandao (Online), badala yake Ofisi ya Waziri wa Kilimo ambayo itakuwa inafuatilia kwa karibu utekelezaji wa utoaji vibali uliofanywa na TFRA.

Hivi karibuni Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA), Dk. Stephan Ngailo, alisema kwa suala la vibali wameshajizatiti kwa kuhakikisha wafanyabiashara wanaoomba vibali wanapatiwa kwa wakati.

"Tunataraji kuanza kuruhusu wafanyabiashara kuomba vibali kwenye kuingiza mbolea, wanapata hati ya kulipia kwa njia ya mtandao na kibali pia.

Alisema kuwa hiyo itarahisisha vibali kutolewa kwa wakati na itaongozeka ufanisi lengo kuhakikisha mkulima anapata mbolea bora, bei rahisi na kwa wakati uliokusudiwa.

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Uhamasishaji muhimu kwa chanjo ya corona

**MWISHONI** mwa mwezi uliopita, Rais Samia Suluhu Hassan alizindua rasmi kampeni ya taifa ya chanjo ya Uviko-19 na kuwa wa kwanza kuchanjwa, kwa lengo la kuuhakikishia umma kuwa chanjo hiyo ni salama.

Baada ya uzinduzi huo wa chanjo, Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Prof. Abel Makubi, anasema, uzinduzi wa utoaji chanjo mikoa yote ulikamilika Agosti 4, mwaka huu.

Katika taarifa yake kuhusu maendeleo ya usambazaji na utoaji wa chanjo hiyo aliyoitoa juzi, anasema, tathmini inaonyesha kuwapo kwa mwitikio mkubwa wa wananchi kupata chanjo hiyo.

Kwa mujibu wa katibu huyo, rekodi ya makundi ya walengwa peke yake, kufikia Agosti 7, mwaka 2021 ilionyesha zaidi ya 164,500 walikuwa wameshajiandikisha kwa ajili ya kupatiwa chanjo wiki hii, huku wengine 105,745 wakiwa tayari wameshapatiwa chanjo kufikia tarehe hiyo.

Sisi tunaunga mkono juhudi zinazofanywa na serikali za kusambaza chanjo hiyo, ili kuhakikisha Watanzania wanaipata kwenye maeneo yao kulingana na maelekezo bila kikwazo chochote.

Hata hivyo, tunadhani kuna haja ya kuongeza jitahada zaidi, ili kusaidia kuongeza idadi ya watu kujitokeza kuchanjwa, kuliko ilivyo sasa, kwani haiendani ya wingi wa Watanzania ambao ni zaidi ya milioni 60.

Tunashauri kuwapo kwa uhamasishaji kila kona ya Tanzania ili watu waone umuhimu wa kwenda kuchanjwa, kwani tunadhani kwamba ukosefu wa elimu ya kutosha kuhusu chanjo unaweza kuchangia hali iliopo sasa.

Si vibaya elimu ikatolewa kwenye minada, vituo vya mabasi na maeneo mengine ya mikusanyiko ya watu ikiwamo hata matamasha ili kuongeza kasi ya watu kwenda katika vituo kwa ajili ya kuchanjwa.

Vilevile, tunadhani hata viongozi wa serikali za mitaa nao wana wajibu wa kutoa elimu katika maeneo yao na ikiwezekana waingie nyumba kwa nyumba ili wananchi wahamasike na kujitokeza kwa wingi.

Tunajua kuwa, kwa namna moja au nyingine, elimu ambayo baadhi ya Watanzania wameipata miaka ya nyuma kuhusu kinga ya corona, inaweza kuwafanya baadhi yao kusita kujitokeza kuchangwa.


Ni kweli suala la chanjo ni hiari, lakini inawezekana wengine wakawa hawajitokezi kuchanjwa kwa sababu tu ya elimu ambayo wamedumu nayo tangu ugonjwa huo ulipoingia nchini.

Kwa mantiki hiyo, tunaona kuna haja kuwapo kwa uhamasishaji unaokwenda sambamba na utoaji wa elimu sahihi kuhusu madhara ya ugonjwa huo na kinga yake ili Watanzania waondokane na 'giza' lililopo.

Tunaamini kwamba hayo yakifanyika idadi ya Watanzania watakaochanjwa itaongezekana na wengine wataendelea kujitokeza zaidi kujiandikisha na kuwa kwenye foleni ya kusubiri kuchanjwa.

Ni kweli huo mwanzo kwa watu waliojitokeza kuchanjwa ni mzuri, lakini tunaamini kuwa kasi zaidi inahitajika, hasa ikiendana na elimu kwa umma kuhusu umuhimu wa kupata chanjo hiyo.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




# Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

## Ndivyo nguvu za wananchi zinavyoinua maendeleo ya elimu

**MAZINGIRA** bora na wezeshi ya kujifunzia na ya ufundishaji kuanzia kuwa na madawati ya kutosha, madarasa yasiyo na msongamano wa wanafunzi vina mchango mkubwa katika maendeleo ya taaluma.

Pamoja na umuhimu huo, shule nyingi nchini zinakabiliwa na tatizo la kutokuwa na mazingira hayo rafiki kwa wanafunzi, ikiwamo pia ukosefu wa mabweni, hali ambayo inaweza kukwamisha wanafunzi kutimiza ndoto zao.

Shule hasa za umma zinakabiliwa na changamoto hiyo, ambayo ni vyema wadau wa elimu kila mmoja kwa nafasi yake kuchukua hatua za kumaliza matatizo hayo ambayo ni ya muda mrefu.

Kwa mfano, kwenye suala la uhaba wa madarasa na madawati, wazazi na walezi wanaweza kushiriki kikamilifu kuzipatia shule samani pamoja na majengo na kuwafanya wanafunzi wasisomee chini ya miti au kurundikana madarasani.

Si hapo tu, bali pia kwenye ujenzi wa mabweni ili kusaidiana wanafunzi wanaoishi umbali na shule, ili waondokane na kero ya kusafiri umbali mrefu kwenda kuafuta elimu au kupanga katika nyumba za uraiani.

Kiujumla, mazingira hayo, si rafiki kwa maendeleo ya elimu kwa wanafunzi, hivyo ni vyema kila upande kufanya sehemu yake ili kuhakikisha wanafunzi wanakuwa katika hali bora ya ujifunzaji na ufundishaji.

Wakati wadau wa elimu wakifanya hayo, serikali kwa upande wake haina budi kuhakikisha shule za umma zinakuwa na walimu wa kutosha kuliko ilivyo sasa ambapo shule inaweza kuwa wanafunzi 500, lakini walimu sita.

Kwa mfano Shule ya Msingi Bulinga iliyoko Musoma Vijijini mkoani Mara, ilianzishwa mwaka 1942 kwa sasa ina wanafunzi 662 walimu saba, huku mahitaji yakiwa walimu 15, madarasa sita wakati yanayohitajika ni 14.

Hali hiyo kwa mujibu wa mwalimu mkuu Alexander Materu, wanafunzi 214 wanasomea chini ya miti, na kwamba, 147 wa darasa la tatu wanatumia chumba kimoja ni dhahiri matatizo ya aina hiyo yatakuwapo kwenye shule nyingi za umma zikiwamo kongwe kama hiyo na kusababisha ufundishaji na ujifunzaji kuwa shida kwa walimu na wanafunzi.

Umefika wakati kamati na bodi za shule kuwa na mikakati ya kushirikisha wazazi na walezi kuchangia maendeleo ya shule ambazo ni mali ya umma kwenye maeneo yao.

Inawezekana wapo baadhi ya watu wanaodhani hawahusiki kwa lolote kuboresha shule hizo, wakiamini kuwa ni kazi ya serikali, lakini ukweli ni kwamba umma unatakiwa kuhudumia shule zake.

Kamati na bodi zinaweza kushirikisha wazazi na walezi kuweka mikakati ya kuhakikisha shule zote zinaondokana na mazingira duni ambayo kwa namna moja au nyingine yanaweza kukwamisha wanafunzi kupiga hatua kielimu.

Katika karne ya sayansi na teknolojia, ni muhimu mazingira ya ujifunzaji na ufundishaji yakaboreshwa badala ya kuendelea kuyafanya kama ya kudumu wakati yanaweza kutatuliwa na jamii kupitia ushirikishwaji.

Jambo la msingi ni kuhamasisha jamii kutambua kuwa shule za umma ni zake, na kwamba zina jukumu la kuzihudumia kadri inavyowezekana badala ya kudhani kuwa hiyo ni kazi ya serikali wakati wote.

Wananchi wakihamasishwa, wanaweza kushiriki katika ujenzi wa vyumba vya madarasa kwa kutoa nguvukazi, iwe kwa kusomba maji, mawe, mchanga na vitu vingine au kuchangia fedha.

Serikali imeshatoa Sh. milioni 40, huku Halmashauri ya Wilaya Musoma ikichangia 5,000,000 na wadau wengine wa elimu kuchangia madawati 46 na vitabu zaidi ya 1,000 na mabati 54.

Fedha hizo kwa mujibu wa mwalimu mkuu huyo, ni kwa ajili ya ujenzi wa madarasa mawili na ofisi ya walimu, huku wadau wengine wakiwa wamejenga choo chenye matundu nane.

Ingawa inaelezwa kuwa wananchi wamehamasishwa na kutoa nguvukazi yao kwenye ujenzi wa madarasa hayo, ni vyema juhudi hizo zikaendelea ili shule hiyo kongwe iwe na mazingira rafiki ya ujifunzaji na ufundishaji.

HABARI KITAIFA

# Hukumu ya Mattaka wa ATCL wiki ijayo

**Na Kulwa Mzee**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, inatarajia kusoma hukumu dhidi ya aliyekuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Ndege Tanzania (ATCL), David Mattaka na wenzake wawili Agosti 20, mwaka huu.

Hukumu hiyo inatarajiwa kusomwa mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi, Janeth Mtega, baada ya kusikiliza ushahidi wa pande zote mbili.

Mattaka na wenzake wanakabiliwa na mashtaka ya matumizi mabaya ya madaraka, kughushi na kuisababishia ATCL hasara ya zaidi ya Sh. bilioni 71.

Wakili wa Serikali, Joseph Kiula, alidai mahakama jana kuwa kesi hiyo ililetwa kwa ajili ya hukumu na wapo tayari.

Hakimu Mtega alisema hukumu haijakamilika, hivyo kesi inaahirishwa hadi Agosti 20, mwaka huu kwa ajili ya kusikiliza hukumu hiyo.

Mbali na Mattaka, washtakiwa wengine katika kesi hiyo ni aliyekuwa Ofisa Mtendaji Mkuu wa Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA), Dk. Ramadhan Mlinga na aliyekuwa Mwanasheria wa Mamlaka hiyo, Bertha Soka.

Washtakiwa wanakabiliwa na mashtaka sita likiwamo la matumizi mabaya ya madaraka na kuisababishia serikali hasara ya zaidi ya Sh. bilioni 71.

Upande wa mashtaka ulikuwa na mashahidi zaidi ya 20 pamoja na vielelezo mbalimbali, huku washtakiwa wakijitetea wenyewe pamoja na mashahidi wao.

Katika kesi ya msingi, Mattaka anadaiwa kuwa Oktoba 9, mwaka 2007, wakati akitekeleza majukumu yake kama Mkurugenzi Mtendaji wa ATCL, alitumia madaraka yake vibaya kwa kusaini mkataba wa kukodisha ndege aina ya Airbus na kwamba, mkataba huo unadaiwa kuisababishia serikali hasara ya zaidi ya Sh. bilioni 71.

Katika shtaka la kughushi, Dk. Mlinga na Soka wanadaiwa kuwa Machi 19, mwaka 2008 katika Ofisi za PPRA zilizopo Wilaya ya Ilala mkoani Dar es Salaam, walighushi muhtasari wa kikao wa tarehe hiyo, wakionyesha kwamba, mamlaka hiyo ilikaa kikao na kujadili maombi ya kuidhinisha ATCL kukodisha ndege.

# Mwanamke auawa kwa kukatwa shingo

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

WATU watatu wamefariki dunia katika matukio tofauti likiwamo la mwanamke wa miaka 70 kukatwa shingo na kitu chenye ncha kali.

Akizungumza na waandishi wa habari, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Pwani, Wankyo Nyigesa, alisema matukio hayo yametokea kati ya Agosti 3 hadi 8.

Alisema katika tukio lililotokea Kijiji cha Kitonga Wilaya ya Bagamoyo, mwanamke mwenye umri wa miaka 70, aliuawa kwa kukatwa shingo na kitu chenye ncha kali akiwa shambani kwake.

Kamanda Wankyo alisema watuhumiwa walimkata mwanamke huyo shingo na kumtenganisha kichwa na kiwiliwili na kisha kutoweka kusikojulikana.

Wankyo alisema msako unaendelea kuwakamata waliohusika na tukio hilo ambao haijajulikana walikokimbilia baada ya kutekeleza tukio hilo.

Katika tukio lingine lililotokea Agosti 8 majira ya saa tisa jioni Kitongoji cha Tobora Kata ya Msata, mtu mmoja mwenye jinsia ya kike (26) mkazi wa Pongwe Msungura alibakwa kisha kuuawa.

Kamanda Wankyo alisema mwili wa mwanamke hiyo uliokotwa vichakani baada ya watuhumiwa kutekeleza mauaji hayo, na kwamba, mtuhumiwa mmoja amekamatwa kuhusiana na tukio hilo.

Wankyo alisema Jeshi la Polisi linaendesha msako kuwakamata watu waliohusika na tukio lingine la mauaji lililotokea Kijiji cha Kwang'andu Kata ya Mbwewe.

Kamanda Wankyo alisema katika tukio hilo, mtu mmoja aliuawa kwa kuchomwa na mkuki akiwa katika shughuli zake za shamba.

Wakati huo huo, mtu mmoja mkazi wa Kibondeni Wilaya ya Kibaha amekamatwa na polisi kwa tuhuma za kukutwa na sare za Jeshi la Polisi.

Kamanda Wankyo alisema mtuhumiwa huyo amekamatwa akiwa na sare za jeshi hilo za kaki pea tatu, mkanda wa bendera mmoja, mkanda wa Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) mmoja, buti pea tatu mbili nyeusi na moja ya kaki, begi dogo na sweta.

Kamanda alisema mtuhumiwa huyo alikamatwa majira ya usiku na kwamba sare hizo anadaiwa kuzitumia katika kazi za kipolisi.



Mfanyabiashara wa samaki wakavu katika Soko Kuu la Iringa, Grey Msungu, akisubiri wateja jana, bei ya Samaki katika soko hilo imepanda kutokana na uhaba wa kitoweo hicho kutoka Bwawa la Mtera. **PICHA: FRANCIS GODWIN**

# Samaki waadimika kisa uvuvi haramu

**Na Francis Godwin,** IRINGA

SOKO Kuu la Manispaa ya Iringa katika Mkoa wa Iringa linakabiliwa na uhaba mkubwa wa samaki wakavu kutokana na msako mkali unaoendelea katika Bwawa la Mtera wenye lengo la kutokomeza uvuvi haramu.

Wakizungumza na Nipashe jana wafanyabiashara wa samaki sokoni hapo, walisema kumekuwapo na uhaba mkubwa wa samaki kwa kipindi cha miezi miwili mfululizo sasa, hali iliyopelekea kupanda kwa bei ya samaki kutoka shilingi 1,000 hadi 2,500 kwa samaki mmoja mdogo.

Mfanyabiashara wa samaki sokoni hapo, Grey Msungu, alisema sehemu kubwa ya samaki walikuwa wakitegemea kutoka Bwawa la Mtera Iringa ila kwa sasa kuna na uhaba mkubwa wa samaki hao na hata wakiletwa hawatoshelezi mahitaji ya wafanyabiashara sokoni hapo.

Msungu alisema sehemu kubwa ya wafanyabiashara wa samaki sokoni hapo wanalazimika kujihimu mapema kwenda kwenye mabasi ya mizigo yanayotokea Mtera ili kujumua mzigo kupitia kwa wafanyabiashara wachache ambao wamekuwa wakitumia usafiri huo, ingawa bado hitaji la samaki ni kubwa.

Hata hivyo, alisema kutokana na Bwawa la Mtera uvuvi kushuka kwa sasa wanategemea samaki kutoka mkoa wa Singida.

Msungu alishauri wafanyabiashara wa mkoa wa Mwanza na maeneo mengine ya Tanzania ambayo samaki ni wengi kuchangamkia fursa hiyo ya kuleta samaki katika soko la Iringa, kwani walaji ni wengi hasa samaki hao wakavu maarufu kama samaki wa Moshi.

Ignasi John ni mmoja kati ya wavuvi wa samaki katika Bwawa la Mtera Iringa, alisema uhaba wa samaki si tu katika soko la Iringa bali hata Mtera hali ya upatikanaji wa samaki ni shida kutokana na wavuvi wengi kushindwa kuingia bwawani kuvua.

# Kimya cha miezi 8 cha wanafunzi kutoroshwa

**Na Thobias Mwanakatwe**

WANAFUNZI wawili wa kidato cha pili katika Shule ya Sekondari Itope iliyoko wilayani Kyela mkoani Mbeya, wanaodaiwa kuroroshwa na mfanyabiashara mmoja wa mjini Kyela, wamemaliza miezi minane sasa bila kupatikana wala kujulikana walipo.

Kutokana na hali hiyo, familia za wanafunzi hao zimeendelea kuwa katika majonzi kutokana na kutofahamu kama huko walipo wapo hai au wameshakufa.

Wazazi wa wanafunzi hao mara zote wamekuwa wakilitupia lawama Jeshi la Polisi Mkoa wa Mbeya kwa ukimya katika kushughulikia suala hilo.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mbeya, Urlich Matei, akizungumza na gazeti hili jana kwa njia ya simu, alisema suala hilo limekuwa gumu kumkamata mtuhumiwa kwa sababu wanafunzi hao walikubaliana na mtuhumiwa huyo.

"Hili suala linakuwa gumu kwa sababu wale watoto wamekuwa wamekubaliana na mhalifu kufanya kosa, sio kwamba hawapo hai, wapo hai wameamua kwenda kuendesha maisha wanakojua wao," alisema Matei.

Kamanda Matei hata hivyo, alisema atawasiliana na polisi wa Kyela kujua kinachoendelea kwa sababu aliyekuwa Mkuu wa Polisi Wilaya ya Kyela (OCD) alihamishwa akapelekwa Zanzibar.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Anna Henga, akizungumza na gazeti hili jana, alisema Mei 16, 2021 walipofanya ziara katika Wilaya ya Kyela mkoani Mbeya kufuatilia sakata la wanafunzi hao, walihakikishiwa na Jeshi la Polisi kwamba watamkamata mtuhumiwa.

"Siku tumekwenda ofisini na kuongea na Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mbeya, alituambia ndani ya mwezi mmoja watahakikisha mtuhumiwa anakamatwa, lakini tunashangaa ni miezi miwili sasa tangu tuonane na RPC hakuna kinachoendelea katika suala hili," alisema Henga.

Henga alisema kutokana na ukimya huo, wameshamwandikia barua RPC Mbeya kumkumbushia suala hilo kujua kinachoendelea, lakini barua yao haijajibiwa.

"Tunashangaa jeshi kubwa linashindwaje kumkamata mtuhumiwa mfanyabiashara huyo wakati ana biashara zake na zinaendelea mjini Kyela kama kawaida... tukiona hakuna kinachoendelea itabidi tuombe appointment (miadi) ya kuonana na Mkuu wa Jeshi la Polisi (IGP) ili atusaidie," alisema Henga.

Wanafunzi hao (majina tunayahifadhi) wanadaiwa kutoroshwa na mfanyabiashara huyo mwenye nguvu ya fedha tangu Januari mwaka huu, lakini ambapo hadi sasa hawajulikani waliko.

Baada ya kutoroshwa, taarifa ziliripotiwa katika Kituo cha Polisi Kyela mjini na kupewa RB namba KY41/RB/07/2021 na ISK/RB/41/2021, lakini tangu taarifa za tukio hilo zitolewe mtuhumiwa hajakamatwa ikiwa ni miezi minane sasa.

Wazazi wa wanafunzi hao kwa muda mrefu wamekuwa wakifuatilia polisi kujua kama mtuhumiwa amekamatwa au watoto wao wamerejeshwa, lakini kimekuwa ni kitendawili kisichokuwa na jibu.

Mmoja wa wazazi wa wanafunzi hao, Simon Mwasitu, alipotembelewa na maofisa wa LHRC, alisema ameshakata tamaa kuendelea kulifuatilia Polisi.

Alisema suala hilo ameamua kulikabidhi mikononi mwa Mungu, kwani hivi sasa limeanza kumletea matatizo ya kifamilia na pia kuishi maisha ya wasiwasi, na kwamba wakati mwingine anafungiwa kwa nje mlango wa nyumba yake na watu wasiojulikana bila kufahamu lengo lao.



Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato (kushoto) na Mwakilishi wa Mkuu wa Wilaya ya Bukoba wakiwa na moja wa mkungu wa ndizi, wakati wa Maadhimisho ya Siku ya Wakulima nchini maarufu Nanenane kwa Mkoa wa Kagera yaliofanyika Uwanja wa Kyakailabwa, wilayani Bukoba mkoani humo mwishoni mwa wiki. **PICHA: ZUWENA MSUYA**

# Wawekezaji wakumbushwa wajibu kwa jamii

**Na Abdallah Khamis,** MTWARA

NAIBU Waziri wa Madini, Prof. Shukrani Manya, amewataka makatibu tawala wa mikoa na wakuu wa wilaya kuhakikisha makubaliano yanayoingiwa kati ya wawekezaji na halmashauri, ya kurudisha huduma za jamii kwa wananchi walio katika maeneo ya uwekezaji yanatekelezwa.

Amesema makubaliano hayo yakitekelezwa na wawekezaji wakitimiza wajibu wao, wananchi watafaidi matunda ya uwekezaji hususan katika sekta ya madini, hali itakayowafanya wazidishe ushirikiano kwa wawekezaji hao.

Prof. Manya alitoa kauli hiyo mkoani Mtwara, akiwa katika siku ya kwanza ya ziara yake ya siku mbili mkoani humo ambapo amekutana pia na wachimbaji wa madini ya chumvi mchanga na dhahabu.

Alisema baadhi ya wawekezaji hawatimizi wajibu wao kama walivyosaini makubaliano ya kurudisha asilimia katika jamii inayowazunguka, hali aliyoeleza inajenga uadui kati yao na wananchi.

"Makatibu tawala wa mikoa na wakuu wa wilaya fuatilieni utekelezaji wa makubaliano kati ya halmashauri na wawekezaji katika kurudisha huduma za jamii kwa wananchi, kwa kuwa baadhi ya wawekezaji hawatimizi makubaliano ipasavyo," alisema Prof. Manya.

Akizungumzia soko la madini ya chumvi, aliwataka wachimbaji wa madini hayo kutumia fursa za soko zinazopatikana katika nchi ya Congo DRC na Burundi.

## Vodacom yazindua kampeni"Kimbiza na 4G ya Ukweli"

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya teknolojia na mawasiliano ya Vodacom Tanzania, imezindua kampeni mpya ya "Kimbiza na 4G ya Ukweli".

Kampeni hiyo iliyozinduliwa jana jijini Dar es Salaam, inalenga kuifahamisha jamii kuhusu kasi na uhakika wa mtandao wake unaowezeshwa na uwekezaji makini katika teknolojia pamoja na upana wa huduma inazotoa kwa wateja wake.

Akizungumza wakati wa uzinduzi huo, kwa niaba ya Mkurugenzi wa Kampuni ya Vodacom Tanzania PLC, Mkurugenzi wa Uhusiano na Mawasiliano, Rosalynn Mworia, alisema Vodacom imekuwa ikiendelea kuwekeza na kuboresha mtandao wake ili kuhakikisha unawapa wateja wake teknolojia ya kisasa pamoja na bidhaa na huduma za kibunifu.

Aliongeza kwamba dhamira hii imezaa mtandao bora wa 4G na wa kuaminika, ulio mpana na wenye kufikia maeneo ambayo wengine bado wanajifikiria kufika. Upana huu wa kipekee pamoja na uwezo kiteknolojia unawapa watumiaji wake huduma bora za sauti, ujumbe mfupi na kupata intaneti yenye ubora zaidi.

Kwa muda mrefu, Vodacom Tanzania imekuwa ikiwekeza kwenye mtandao kwa kiwango kikubwa kuliko kampuni zingine za mawasiliano na sasa inamiliki zaidi ya minara 3,500 ya 2G, zaidi ya 3,000 ya 3G na zaidi ya 2,000 ya 4G, jambo ambalo linaipa Vodacom mtandao mpana zaidi na wenye kasi zaidi. Mtandao huu unawafikia asilimia 92 ya wananchi.

Katika hafla hiyo, ilielezwa kuhusu matokeo chanya ya mtandao huo kwa jamii, na kwamba matokeo haya yametokana na dhamira ya kampuni ya Vodacom kutimiza mkataba wake na jamii.

Akifafanua zaidi jinsi mtandao wa Vodacom unavyowawezesha watumiaji wake, Mworia alisema: "Vodacom Tanzania ina mpango wa kuhakikisha taifa zima linakuwa na jamii inayozingatia ujuzi na uelewa kupitia matumizi ya TEHAMA, wakati huohuo tukipunguza utofauti kati ya upatikanaji wa mawasiliano pamoja na kuboresha huduma zetu za data na sauti.

"Dhamira hii imetupelekea kuongeza idadi ya huduma zetu kwa wateja mpaka kufikia sehemu sasa tunatoa huduma anuwai zaidi ya mawasiliano peke yake."

Katika mkutano huo, pia kulikuwa na fursa kwa waliohudhuria kujionea teknolojia na huduma za Vodacom, ambapo pia Mkurugenzi wa Uhusiano na Mawasiliano aliwahamasisha watumiaji wa Vodacom kuendelea kutumia mtandao huo na kwa ambao hawajajiunga kufanya hivyo ili kujionea ubora wa mtandao unaoaminika.

# Wadai kulazimika kutumia bodaboda kusafirisha fedha

**Na Richard Makore,**
MWANZA

BAADHI ya wananchi wakiwamo wafanyabiashara jijini Mwanza wamebuni njia mbadala ya kusafirisha fedha kutoka sehemu moja kwenda nyingine kwa kutumia madereva wa pikipiki (bodaboda), badala ya kutuma fedha kwenye simu kwa madai kwamba wanakwepa makato makubwa ya miamala.

Wamesema mfanyabiashara anapata hasara anapotuma Sh. milioni 1 kulipia bidhaa dukani kwa kuwa mpokeaji atakatwa Sh. 30,000 badala yake anamlipa dereva wa bodaboda Sh. 2,000 ili kumpelekea kiasi hicho cha fedha kutoka sehemu moja kwenda nyingine.

Mfanyabiashara wa vinywaji vya jumla aina ya pombe, Muatafa Misifa akizungumza na Nipashe jana alisema anapokea fedha nyingi za wateja kwa kupelekewa na bodaboda tofauti na huko nyuma.

Alisema bodaboda ambao ni waaminifu wamekuwa wakifanya biashara ya kusafirisha fedha husussani kwa wafanyabiashara.

Aliongeza kuwa njia hiyo siyo salama kwao, lakini wanona ni afadhali kwa kuwa wanatumia fedha kidogo, lakini wanasafirisha fedha nyingi mpaka Sh. milioni 3 kwa gharama isiyozidi Sh. 5,000.

Mkazi mwingine wa Jiji la Mwanza, Faustine Hosea, alisema biashara ya kusafirisha fedha kwa bodaboda imeanza kushika kasi badala ya kutumia simu za mkononi.

Alisema watu wengi kwa sasa kama yupo jijini Mwanza anampatia bodaboda Sh. 1,000 anampelekea zaidi ya Sh. 500,000 kutoka sehemu kwenda kwenda nyingine.

Alisema bodaboda ambao ni waaminifu na ambao wanajulikana kwa sasa wanapata kazi hizo na kwamba wanazifurahia zaidi kuliko kubeba abiria.

Mmoja wa bodaboda, Salum Mwilazi, alisema kazi hiyo inawalipa kwa sasa kwa kuwa wanatumiwa na watu wengi kuwasafirisha fedha ingawa alisema wanakuwa katika hatari ya kuvamiwa na kuporwa kama fedha ni nyingi.

Alisema katika vijiwe vyao wamekubaliana kufanya kazi kwa uaminifu ili wananchi waendelee kuwaamini na kuwatumia badala ya kufanya vitendo vya wizi na kutoroka na fedha za wateja wao.

Kwa upande wake, mfanyabiashara wa dagaa katika soko la Mwaloni, Robison Kairuki, alisema yeye anawatumia madereva wa boti zinazokwenda visiwani badala ya kutuma fedha kwenye simu.

Alisema akimpa dereva Sh. milioni 5 kenye bahasha anamlipa Sh. 10,000 na fedha hizo zinamfikia mlengwa huko visiwani kwa ajili ya kumnunulia dagaa, lakini akizituma kwa simu makato yake ni makubwa zaidi.

Akizungumzia utaratibu huo, Kamanda wa Polisi mkoani Mwanza, Ramadhani Ng'anzi, alisema hajapokea malalamiko ya bodaboda kukimbia na fedha za watu wanazosafirisha kutoka sehemu moja kwenda nyingine.

Kamanda Ng'anzi alisema Jeshi la Polisi mkoani Mwanza, limeendelea kutoa elimu kwa bodaboda kujiepusha kutumika kutenda uhalifu wa namna yoyote.

Hata hivyo, kamanda Ng'anzi aliwataka wananchi kutumia njia yenye usalama zaidi kutuma fedha ikiwamo benki na simu za mkononi kuliko kuwapatia bodaboda kwa kuwa ni hatari kwao na wanaweza kuibiwa kirahisi.

"Hatujapokea malalamiko yoyote ya kuibiwa fedha na bodoboda, labda ni kwa sababu ya elimu tunayowapa bodoboda ama kutokana na kuimarika kwa doria mtaani, lakini niwaombe wananchi watumie njia rasmi na salama ikiwamo simu za mkononi na benki badala ya kuwapatia fedha nyingi bodaboda wazipeleke sehemu," alisema.

Alisema kusafirisha fedha kupitia bodaboda ni gharama rahisi, lakini ni hatari kwa sababu mtu anaweza kuibiwa kirahisi.



Vijana wa Jimbo la Masasi mkoani Mtwara wakiwa wamekusanyika wakati walipokuwa wakisubiri kukabidhiwa rasmi pikipiki zao ambazo wamekopeshwa na Mbunge wa Jimbo hilo, Geofrey Mwambe, ambapo vijana 25 wamekopeshwa pikipiki hizo na kukabidhiwa rasmi jana mjini Masasi. **PICHA: HAMISI NASRI**

# Kiwanda chasitisha uzalishaji wa mafuta

**Na Beatrice Shayo**

KIWANDA cha kutengeneza mafuta ya kula ya alizeti cha Yaza Investment Company Limited kilichopo mkoani Singida, kimesitisha uzalishaji kwa muda usiofahamika hadi kitakapotatua vikwazo kadhaa.

Hayo yalisemwa na Mkurugenzi Mkuu wa Kiwanda cha Yaza, Yusuph Nalompa, wakati akitoa taarifa kwa waandishi wa habari kuhusiana na kusitisha uzalishaji wa mafuta kutokana na sababu zilizo nje ya uwezo wao.

"Wateja wetu na Watanzania kwa ujumla tunawajulisha kwa sasa kampuni yetu haizalishi mafuta ya kupikia ya alizeti yanayotambulika kwa nembo ya "halisi" kwa sababu zilizo nje ya uwezo wao," alisema Nalompa.

Nalompa alisema mafuta yoyote ya kupikia yanayosambazwa nchini na nje ya nchi yenye nembo ya "halisi" hayajazalishwa na kampuni yao, hivyo wananchi waepukane na matapeli.

"Kama kuna watu wanazalishaji mafuta hayo na kuweka nembo ya 'Halisi' ambayo ni mali ya kampuni yetu basi watakuwa wameghushi bila kupata idhini ya mmiliki kinyume cha kifungu cha 32 cha sheria ya biashara na huduma," alisema.

"Tunawaonya wale wote wanaosambaza mafuta hayo kwa kughushi nembo ya "halisi" waache mara moja, hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yao," alisisitiza Nalompa.

Aidha Nalompa amewatahadharisha wateja wao na wananchi kwa ujumla kuwa kampuni yao haitahusika kwa njia yoyote ile na madhara yatakayompata mlaji au muuzaji wa mafuta hayo ambayo hayawazalishi kwa sasa.

Kiwanda hicho kimesitisha uzalishaji huo wakati kukiwa bado kuna ongezeko la bei ya mafuta ya kula katika masoko mbalimbali ya hapa nchini.

# Wanafunzi wajengewa sekondari eneo lao

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

WANAFUNZI waliokuwa wakitembea umbali mrefu kwenda na kurudi shuleni katika kijiji cha Mega Halmashauri ya Msalala wilayani Kahama mkoani Shinyanga, wameondokana na kero hiyo, baada ya kujengwa shule mpya ya sekondari eneo hilo.

Mkuu wa Shule ya Sekondari ya Mega, Revocatus Masembo, alibainisha hayo mwishoni mwa wiki katika ziara ya Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Dk. Philemon Sengati, kwa ajili ya kukagua màendeleo ya shule hiyo.

Alisema kujengwa kwa shule hiyo kumesaidia kuwapunguzia adha wanafunzi kutembea umbali mrefu kwenda kata jirani ya Segese.

Wanafunzi hao walikuwa watembea umbali wa kilomita 8 kwenda shule na kusababisha baadhi yao kukatisha masomo ikiwamo kupewa ujauzito.

"Shule hii mpya ya sekondari Mega, imeanza kutoa elimu mwaka huu, na tuna jumla ya wanafunzi wa kidato cha kwanza 82, wasichana 56, wavulana 26, na vyumba vya madarasa vipo vinne pamoja na maabara za sayansi kwa ajili ya wanafunzi kusoma kwa vitendo," alisema Masembo.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Dk. Philemon Sengati, alisema serikali ilianzisha ujenzi wa shule hiyo mpya kwa kushirikiana na nguvu za wananchi baada ya kuona wanafunzi wanateseka kufuata masomo umbali mrefu.

Aidha, alisema suala la ukosefu wa huduma ya umeme na maji kwenye shule hiyo atalishughulikia ili kuhakikisha wanafunzi wanasoma katika mazingira mazuri na kupata elimu bora.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Mkoa wa Shinyanga, Mabala Mlolwa, alisema ujenzi wa shule hiyo ni utekelezaji wa ilani ya chama hicho, kwa kuhakikisha wanafunzi wanapata elimu katika mazingira rafiki.

# Wanawake waliogombea mwaka 2020 wapewa mbinu

**Na Mwandishi Wetu,** PEMBA

WANAWAKE waliogombea mwaka 2020 wamesema ili kuhakikisha wanafikia asilimia 50-50 kwenye vyombo vya kutoa maamuzi, ni vyema wakashirikiana kuanzia ngazi ya jimbo hadi kwenye jamii.

Wakizungumza katika mkutano wa tathmini baada ya kumaliza uchaguzi mkuu mwaka 2020 uliofanyika Wete, walisema, wanawake hukosa mashirikiano kuanzia kwenye ofisi zao za jimbo, jambo ambalo linawarudisha nyuma. Walisema kuwa, kumekuwa na fitina za chini kwa chini kwamba mwanamke hafai kuwa kiongozi na hatimaye kuwashawishi wajumbe wasimpe kura, jambo ambalo linawavunja moyo katika harakati hizo za kugombea nafasi za uongozi.

"Kwa kweli shida inaanzia kwenye ofisi za majimbo yetu, wale viongozi huwashawishi wajumbe wasimpe kura mwanamke, wanasema hatuwezi lolote kazi yetu ni kupika tu," walisema wagombea hao.

Walieleza kuwa ipo haja kwa viongozi wa majimbo kupewa elimu, ili wachague mtu kwa utendaji wake na sio kwa kuwa anajulikana sana, kwani hawatofikia lengo la kutatua changamoto zinazowakabili wananchi.

"Mimi ni mtendaji mzuri sana na utendaji wangu unaonekana kila mahala, lakini nilipoamua kugombea niliambiwa wewe mwanamke nenda kazae tu, wanaosema hivyo ni viongozi wetu," alisema mgombea Asha Omar Said.

Mgombea Riziki Abdalla Omar alieleza kuwa, wamekuwa wakijitahidi kuingia kwenye kinyang'anyiro cha kugombea uongozi ingawa fitina za viongozi wao ndio zinazowaumiza.

"Wanawake tunajiamini na tunasimama imara kutetea haki yetu, lakini kwa hali tunayofanyiwa na viongozi wetu, maisha hatutofika mbele, maana wao ndio wanaohamasisha wajumbe tusipigiwe kura," alieleza.

Naye mgombea Faida Juma alisema kuwa, kitu chengine kinachowavunja moyo ni kuona kwamba wanawake wenzao ndio ambao wanawadharau na kuwakebehi na hatimaye kuwawekea chuki zisizo na msingi.

Amira kutoka Jimbo la Gando, Salma Khamis Juma, alieleza kuwa kutambulika ni jambo muhimu sana, hivyo kuanzia sasa wanawake wachukue jitihada za kuwa karibu na jamii, ili watakapogombea uongozi iwe tayari imeshawakubali.

"Wanawake ni watu wa huruma, tuna imani, hivyo tutakapoingia kwenye vyombo vya kutoa maamuzi tutaisaidia jamii kutatua changamoto mbalimbali zinazowakabili," alisema.

Asy Amour Abraham kutoka Jimbo la Wete, alisema pamoja na changamoto zilizowakabili katika chaguzi zilizopita, sasa ni wakati wa kujipanga upya, ili kuhakikisha ifikapo mwaka 2025 wanaingia majimboni kuusaka uongozi.

"Tumtegemee Mungu katika mambo yetu, yeye ndie mwenye uwezo wa kukupa, hivyo tusikate tamaa, kipindi kilichopita haikuwa riziki yetu sasa tujiandae kwa baadaye," alisema.

Mratibu wa Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania ( TAMWA)- Pemba, Fat-hiya Mussa Said, alisema ili chaguzi zijazo wajitokeze kwa wingi kugombea uongozi, kuna haja ya kukaa pamoja na kuandaa mikakati ambayo itawasaidia.

Mkutano huo ambao umewashirikisha viongozi wanawake waliofanikiwa na ambao waliogombea na hawakufanikiwa, ulikuwa na lengo la kujitathmini baada ya kumaliza uchaguzi mkuu wa mwaka 2020.



Kijana Livinus Misango, akiendesha trekta lake alilobuni na kuunda kwa kutumia teknolojia ya kienyeji kwa ajili ya kilimo shambani, huku akiwa amebeba vijana wenzake nyuma. **PICHA: ANTHONY GERVAS**

# Tigo yawaandaa wanafunzi kuajiriwa

**Na Elizabeth Zaya**

KAMPUNI ya simu za mkononi ya Tigo, imeanzisha programu ya kuwaendeleza wahitimu kuchangamkia soko la ajira.

Mkurugenzi Mtendaji wa Tigo, Simoni Karikari, alisema kwamba kupitia programu hiyo itawasaidia wawe na nafasi nzuri ya ushindani wa kuajirika.

"Kutokana na ushindani wa ajira uliopo, ambao umesababishwa na kutokuwa na uwiano sahihi kati ya kazi zilizopo na idadi ya wahitimu wanaotafuta ajira, wanafunzi wanazidi kukabiliana na shinikizo la kuboresha sifa zao za kitaaluma pamoja na kuongeza ujuzi wenye manufaa," alisema Simoni.

"Changamoto kubwa inayochangia wahitimu wengi kushindwa kushindana katika soko la ajira ni kutokana na kukosa ujuzi wa ziada wa kuwawezesha kupata ajira katika sekta rasmi. Ujuzi unajumuisha uchambuzi, utaalam, ujasiriamali, usimamizi, utunzaji wa muda na ujuzi wa msingi wa maarifa ya matumizi ya komputa."

Alisema kupitia program hiyo itawasaidia kupata uzoefu wa mambo ya muhimu ikiwamo yanayohusu utendaji wenye ufanisi katika masuala ya msingi, kwenye sekta ya ajira.

"Mkakati ambao kampuni hii ya mawasiliano ya simu inalenga ni kusajili wahitimu wapya kutoka katika vyuo vikuu nchini na nje ya nchi kwa lengo la kutaka kuwakuza na kuwaonyesha maisha halisi, mazingira ya kazi kwa dhumuni la kuwaandaa na kuwapatia fursa ya kujipatia ujuzi,"alisema Simoni.

"Na programu hii inayoendeshwa na Tigo kwa wahitimu wapya katika kuwajumuisha katika kampuni, inafanywa kwa mwaka mmoja na inaamini katika kipindi hicho wanakuwa wamejifunza shughuli zote zinazohusiana na biashara ya mawasiliano ya simu pamoja na kuelekeza nguvu katika kukuza ujuzi wao, kwenye masuala ya msingi wanayopendelea wao."

Pia, alisema kupitia program hiyo, watakuwa wanapatiwa ushauri wa kitaaluma.

"Na tunaamini kwamba, programu hii itakuza kwa kiwango kikubwa ujuzi wao kupitia mafunzo na ushauri, ambao unahitajika katika kuwaandaa, kwa ajili ya ajira baadae na nafasi za uongozi katika ulimwengu wa mashirika ndani na nje ya nchi,"alisema Simoni.

# Washauriwa kutumia ithibati ya Tanzania

**Na Joseph Mwendapole**

WAFANYABIASHARA wameshauriwa kutumia ithibati ya Tanzania badala ya kwenda kuitafuta nje ya nchi kama ilivyokuwa zamani.

Hayo yalisemwa jana na Katibu wa Kampuni ya MICO Halal International Certification Bureau ya Tanzania, Sheikh Jumanne Kasonso, wakati akizungumzia umuhimu wa bidhaa zenye ithibati ya Halal kwenye ofisi za kampuni hiyo jengo la Butiama Magomeni jijini Dar es Salaam.

MICO ndiyo wakala wa Halal wa Baraza Kuu la Waislamu (BAKWATA) ambayo imepata cheti cha kimataifa kwa ajili ya kutoa ithibati ya Halal kwa bidhaa zinazotumika nchini na zile zinasafirishwa kwa ajili ya kuuzwa nje ya nchi.

"Halal ni kitu kilichoruhusiwa kisheria ambacho hakina madhara kwa binadamu ili bidhaa iwe Halal lazima ikidhi vigezo au viwango vya nchi husika mfano TBS na baada ya kukidhi vigezo hivyo ikidhi pia vigezo vya kisharia (dini)," alisema.

Hivi karibuni MICO International Halal Bureau of Certification ilipata cheti cha kimataifa kitakachoiwezesha kutoa ithibati ya Halal kutoka kampuni ya Hafsa Halal Certification and Food Import and Export Limited ya Uturuki.

Kuhusu umuhimu wa bidhaa kupata ithibati ya Halal alisema cheti hicho hutolewa na Bodi ya Halal ambayo imekidhi viwango vya Halal kimataifa.

Alitaja faida za kupata cheti cha Halal kuwa ni bidhaa kukubalika katika masoko ya kimataifa hasa nyama kwenye masoko ya Uarabuni na Asia ambako hawakubali bidhaa isiyo na ithibati ya Halal kutoka taasisi iliyokidhi viwango vya kimataifa.

Alisema kwa MICO kupata cheti hicho cha Halal kimataifa kwa mara ya kwanza sasa Tanzania itakuwa na kampuni iliyokidhi viwango vya kimataifa vya ithibati ya Halal.

"Kwa sasa MICO ndiyo kampuni pekee hapa nchini yenye uwezo wa kutoa ithibati ya Halal kimataifa katika bidhaa zote Halal nchini iwe nyama au bidhaa zingine na tunaomba wananchi watumie bidhaa zenye ithibati ya Halal kwa afya zao," alisema Sheikh Kasonso.

Alitaja faida nyingine kuwa ni bidhaa za Tanzania hususan nyama kukubalika kwenye soko la kimataifa kama uarabuni na barani Asia ambako huwa hawakubali bidhaa ambayo haina nembo ya Halal.

Alisema cheti hicho kitasaidia kuipatia nchi fedha za kigeni kwani kampuni za ndani zitakuwa na uwezo wa kusafirisha bidhaa mbalimbali ikiwamo nyama kwenye mataifa mbalimbali duniani."

Nipashe
# TESA
Jumanne Agosti 10, 2021
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI



Ukurasa 12

**DC Shinyanga anapomaliza machungu walimu shuleni**



Ukurasa 13

Vituo vya umahiri viing'arishe Tanzania visiishie kuwa hadithi



**NIDA ni maji shingo vitambulisho vya utaifa**

Ukurasa 14

ELIMU

NA MARY GEOFREY

# MABINGWA AFYA WAONGEZA UHAKIKA CHANJO

■ Watoa hofu kuganda damu, wasema haijaripotiwa nchini
■ Washauri kuacha kunywa siku kadhaa kabla na unapochanja

WAKATI Watanzania wakiendelea kupata chanjo ya UVIKO-19 katika vituo maalumu nchini kote, wataalamu na mabingwa wa afya , wanawahimiza wananchi kuchanja na kupuuza sintofahamu kwenye jamii, ambayo inaweza kuwa chanzo cha hofu kwa baadhi ya watu.

Tanzania imepokea msaada wa chanjo aina ya Johnson & Johnson Jensen kutoka Marekani mwezi uliopita iliyozinduliwa na Rais Samia Suluhu Hassan, kwa kuchanjwa na kuongoza viongozi wa serikali na wa dini kuchanja.

Licha ya kuanza kutolewa kwa chanjo hiyo, imezuka sintofahamu kutoka kwa wananchi ambayo inaweza kutia hofu, kwa baadhi ya watu kutokuchanja.

Katika kuelimisha jamii, wataalamu wa Wizara ya Afya,, wanakutana na wanahabari mwishoni mwa wiki iliyopita kujibu hoja mbalimbali.

Mkurugenzi wa Kuratibu Utafiti wa Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu nchini (NIMR), Dk. Paul Kazyoba, anapojibu hoja zinazowatatiza wananchi kama hisia kuwa inaongeza nguvu za kiume, unywaji pombe, muda inapoanza kufanya kazi, akizungumzia pia madhara na faida zake, anaanza na nguvu za kiume.

**NGUVU ZA KIUME**

Dokta Kazyoba anasema hakuna uhusiano kati ya chanjo na kuongezeka nguvu za kiume huo ni uzushi na kuongeza kuwa hakuna utafiti uliofanywa kuhusu uhusiano wa chanjo ya Johnson & Johnson inayotolewa nchini na kuongeza au kupunguza nguvu za kiume.

"Licha ya kuwa hakuna utafiti kwa sisi wanaume tuliochanja binafsi sikuona mabadiliko yoyote kuhusu nguvu za kiume, kwa maana hiyo naweza kusema chanjo hii haina uhusiano na suala hili," anasisitiza.



Mkuu wa Skuli ya Tiba Chuo Kikuu Cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili (MUHAS), Prof. Projestine Muganyizi, akichanjwa chanjo ya UVIKO-19. **PICHA: MUHAS.**

**HAMU YA POMBE**

Kuhusu unywaji wa pombe, mtaalamu huyo anasema inashauriwa kuwa anayetaka kuchanja asiguse pombe kwa siku tatu kabla na baada ya kuchanja.

"Ni ngumu kumdhibiti mtu mmoja mmoja asinywe pombe, lakini ni muhimu wakazingatia hili hasa kwa vile ikizingatiwa kuwa chanjo haifanyi kazi kwenye mwili wa binadamu mara tu baada ya kuchanja," anasema Dk. Kazyoba.

Anafafanua kuwa mgonjwa anayekiuka masharti na kunywa pombe kabla na baada ya kuchomwa chanjo, yupo katika hatari ya kupata madhara kwenye ini.

Anasema kwa sababu ini lina kazi ya kuchuja sumu katika mwili wa binadamu hulazimika kuanza kupambana na sumu ya pombe wakati huo huo kupokea chanjo inayoingia mwilini.

**ELIMU KUHAMASISHA INAHITAJIKA**

Aidha, mbobezi wa Magonjwa ya Ndani na Bingwa wa Figo, Jonathan Mngumi, anasema idadi ya wagonjwa nchini meongezeka hospitalini hivyo ni muhimu wananchi wakaendelea kupata chanjo na waondoe hofu.

Watanzania wanapaswa kuendelea kuelimishwa kuhusu umuhimu wa chanjo, ili waendelee kupata huduma hiyo na kuipunguzia serikali mzigo mkubwa wa matibabu.

Anasema wataalamu wanaendelea kutoa elimu kwa jamii, kujibu maswali ya wananchi, ili wanaopata chanjo wawe na ufahamu wa kutosha na ikitokea amepata shida yoyote aweze kutoa maelezo.

Anasema elimu ikiendelea kuenea maeneo mbalimbali kwa wananchi ni wazi kuwa idadi ya watakaokuwa wanaendelea kuchanja itaongezeka.

"Ndiyo maana leo tumekutana nanyi hapa leo kusaidia kuielimisha jamii, licha ya kuwa jukumu letu ni kutibu, pia ni kuhakikisha tunawakinga watu wasipate magonjwa," anasema Dk. Mngumi.

**HOFU YA KUGANDA DAMU**

Akizungumzia suala hilo, Dk. Mngumi anaeleza kuwa athari za kuganda kwa damu kwa watu wanaochoma chanjo hiyo inaweza kutokea kwa asilimia 0.0003 na ambao walionekana awali utafiti uilionyesha walikuwa na shida nyingine zilizosababisha shida hiyo na kuongeza kuwa kama ikitokea aliyechoma chanjo akapata tatizo hilo, japo hapa Tanzania hali hiyo haijaripotiwa, inatibika

Anasema kila chanjo ina aina yake ya madhara na kwamba wataalamu wanaona kuwa athari zake ni kidogo ikilinganishwa na faida zinazopatikana.

Dokta Mngumi, anazitaja baadhi ya athari za chanjo anazoeleza kuwa ni ndogo ndogo mfano maumivu kwenye eneo alilochomwa, kuchoka kidogo na homa na kuongeza Mamlaka ya Chakula na Dawa (TMDA) inafuatilia kwa ukaribu taarifa za waliochanjwa na kuwataka wananchi waendelee kujilinda na ugonjwa huo kwa kuzingatia ushauri wa Wizara ya Afya.

"Pia wagonjwa wenye magonjwa sugu ya figo wanashauriwa wapate chanjo hii, ili kuwalinda na UVIKO -19 , chanjo itawalinda hata baada ya kupandikizwa figo," anashauri.

**CHANJO KUANZA KAZI**

Daktari Bingwa wa Magonjwa ya Ndani na Mbobezi wa Moyo katika Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI), Tatizo Sanga, anasema chanjo huanza kufanya kazi kwenye mwili wa mtu kuanzia siku saba hadi 15.

Anasema baada ya mtu kuchoma chanjo mwili huanza kujipanga kutengeneza utaratibu wa kuipokea jambo linalofanyika ndani ya wiki mbili.

Anasema wakati mtu anapata maudhi madogo madogo yanakuwa ni mashambulizi kati ya kinga za mwili na chanjo inayoingia ndani ya mtu.

"Hiki kinakuwa ni kitu kipya kimeingia kwenye mwili wa binadamu ndiyo maana aliyechoma ataanza kusikia dalili za maudhi fulani fulani kutegemea na mwili wake," anasema Dk. Sanga.

**MAGONJWA SUGU**

Kuhusu watu wenye magonjwa sugu kupata chanjo anasema ni muhimu, ili kuwaepusha na mashambulizi ya UVIKO-19 yanayoweza kuwaweka katika hatari tofauti na wasiyo na magonjwa hayo.

"Watu wenye matatizo ya moyo ni muhimu kupata chanjo, ili waepuke changamoto ya upumuaji inayoongeza shambulizi kwenye mwili na kuleta uwezekano wa mgonjwa kupoteza maisha," anasema Dk. Sanga.

Anafafanua kuwa ni hatari zaidi kwa mtu mwenye magonjwa yasiyoambukiza kama moyo, figo na kisukari wanapopata maambukizi wanakuwa katika hatari ya kupoteza maisha.

"Ndiyo maana tunatoa elimu na kushauri wenye magonjwa sugu kupata chanjo, ili kujikinga na hatari hii," Anasisitiza.

INAENDELEA UK.12

ELIMU

NA MARCO MADUHU, SHINYANGA

# DC Shinyanga anapomaliza machungu walimu shuleni

## • Ni ya kukosa samani, 'kushea' na wanafunzi




DC Mboneko akiwakabidhi walimu samani za shule. **PICHA: MARCO MADUHU.**

WANAFUNZI kufaulu na kuendelea vyema kitaaluma kunahusisha juhudi za ufundishaji na ujifunzaji, mazingira wezeshi kama miundombinu ya nje, ya ndani ya madarasa, chakula na utayari wa walezi na wazazi kufanikisha malengo ya kuwapa watoto elimu bora.

Baada ya mzazi na mlezi, wahusika mkuu wa kufanikisha elimu ni walimu ambao wanahitaji mazingira rafiki ya kufundisha, kupunguziwa changamoto zinazowakabili na kuhakikishiwa maslahi bora.

Mwalimu anapoona mazingira ya shule anayofundishia ni rafiki kwake, ni lazima ajitume kufanyakazi kwa bidii, ili kuwafaulisha wanafunzi na kutimiza ndoto zao, huku yeye akijipatia sifa zaidi kutoka kwa wazazi, walezi, wanafunzi na hata taifa kwa kuheshimika na kutuzwa kama mfanyakazi bora.

Vivyo hivyo mwalimu anapokuwa katika mazingira mabovu, anakosa ari ya kufundisha, tena na wengine huomba kuhamishwa, ili waende kwenye shule nyingine, ambazo zina mazingira wezeshi na motisha kwao na shule inayokimbiwa inakabiliwa na upungufu wa walimu na matokeo yake ni kufanya vibaya kwenye matokeo ya mtihani.

Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga, Jasinta Mboneko, katika kuwalinda na kuwahamasisha walimu kufanyakazi kwa dhati na bidii, anasema mazingira wezeshi na vitendeakazi kwa walimu ni sehemu ya motisha na amezipatia viti na meza za kisasa ofisi za walimu wilayani hapo, ili waache kutumia samani za wanafunzi.

> "Sekondari ya Mwawaza wamepata meza nne na viti nane kama nilivyo ahidi, Ngokolo viti viwili na meza 12, nitakwenda kwenye shule nyingine zote ni kuhakikisha walimu wanafanyakazi katika mazingira rafiki na kuongeza ufaulu ,"anasema Yasinta.

Anasema anachukua hatua hiyo, akifahamu kuwa ana jukumu la kutatua changamoto za wanafunzi pamoja na walimu na kukumbusha kuwa mara nyingi walimu wanasahaulika kwa vile wadau wanaegemea zaidi kwa wanafunzi.

"Sekondari ya Mwawaza wamepata meza nne na viti nane kama nilivyo ahidi, Ngokolo viti viwili na meza 12, nitakwenda kwenye shule nyingine zote ni kuhakikisha walimu wanafanyakazi katika mazingira rafiki na kuongeza ufaulu ,"anasema Yasinta.

"Niwahakikishieni serikali itaendelea kuboresha maslahi ya walimu, hivyo naomba mjitume kufundisha kwa bidii na kuondoa matokeo 'F', ningependa wote wafaulu," anaongeza .

Mkuu wa Sekondari Ngokolo, Malale Masali, anasema shule hiyo ina walimu 37, wakiume 27 na waliobakia 10 ni wanawake na kwamba walikuwa na upungufu wa viti viwili na meza 12, lakini sasa wameachana na tatizo la kutumia samani za wanafunzi.

"Tuna muahidi Mkuu wa wilaya, katika matokeo ya mwaka huu 2021 ya kidato cha nne, tutapunguza matokeo F shuleni hapa na kuongeza ufaulu kwa wanafunzi," anasema Masali.

Ernest Mpanda ni mwalimu wa Ngokolo anayeishi na ulemavu wa miguu, anasema awali alikuwa na tatizo la sehemu ya kuhifadhi vitabu, kuandaa kazi na kuzisahihisha pamoja na kufanyia kazi, kwa sababu alikuwa akitumia samani za wanafunzi ambavyo siyo rafiki, lakini sasa amepata kiti na meza na kuahidi kufanyakazi kwa ufanisi.

Mkuu wa Shule ya Sekondari Mwawaza Manispaa ya Shinyanga Juliana Limbe, anasema shule hiyo ina walimu 11 na wamepata viti nane na meza nne, kwa ajili ya matumizi ya walimu.

"Shukrani ya Sekondari ya Mwawaza ambayo tutampatia Mkuu wa wilaya, ni kufanya vizuri katika matokeo ya kidato cha nne mwaka huu, kwa kuongeza ufaulu mkubwa wa wanafunzi,"anasema Limbe.

Diwani wa Kata ya Mwawaza, Juma Nkwabi, anasema hatua ya Mkuu wa Wilaya kutatua changamoto ya walimu ya upungufu wa samani wataendelea kushirikiana na viongozi, walimu na Baraza la Madiwani, ili kutatua changamoto za sekta hiyo inayotoa dira ya maisha ya Mtanzania.

"Napongeza Mkuu wa Wilaya kwa kazi anayoifanya ya kusaidia kutatua changamoto za walimu kwa kuwapatia viti na meza, nawataka wadau wengine wamuunge mkono kwenye hatua hiyo, ili walimu wawe na motisha kwa sababu serikali hatuwezi kuzimaliza shida zao peke yetu kwa uharaka bila kuungwa kushirikiana na wengine,"anasema Mkumbo.

Aidha, anasema katika matokeo ya mtihani kuhitimu kidato cha nne mwaka jana mkoani Shinyanga, wanafunzi waliofanya mtihani huo walikuwa 12,075, miongoni mwao waliopata daraja la kwanza 727, daraja la pili 1,659, la tatu 1,914, la nne 5,898, na waliopata zero 1,877 ufaulu huo ukiwa sawa na asilimia 83.4.

# MABINGWA AFYA WAONGEZA UHAKIKA CHANJO

INATOKA UK.11

**KUSHAMBULIA MAPAFU**

Pauline Chale, Bingwa wa Magonjwa ya Ndani na Mbobezi wa Mapafu na Mahututi, anasema virusi vya UVIKO-19 husababisha madhara kwenye mapafu.

Anasema kuna milango ipo kwenye mapafu, moyo, ini na mfumo wa tumbo ambayo ugonjwa huitumia kujishikiza hadi kufika kwenye seli za damu.

Anasema kutokana na muingiliano huo wa kirusi mgonjwa hubanwa mapafu na kushindwa kuvuta hewa na ndiyo sababu ya kumuwekea hewa ya oksijeni ambayo hutumia hadi wiki nne, ili kurejea katika hali ya kawaida.

"Kutokana na kuwa mgonjwa anakaa kwenye oksijeni kwa wiki mbili hadi nne kama hatapoteza maisha, hutumia mitungi mitatu hadi mitano kwa siku. Wakati gharama ya kumlaza mgonjwa mmoja kwa siku ni Sh. 500,000 hivyo utaona gharama zilivyo kubwa kwa mgonjwa anayeugua UVIKO-19," anasema Dk. Pauline.

Anafafanua zaidi kuwa, mitungi ya gesi inaadimika kwa sababu ya idadi ya aina ya wagonjwa wa mahututi kuongezeka.

Anawataka wananchi kuendelea kujikinga na kupata chanjo kwa manufaa yao binafsi na vizazi vyao.

**WAJAWAZITO, WANAONYONYESHA**

Bingwa wa Mapafu, Grace Shayo, anahimiza wanawake wanaonyonyesha na wajawazito kuendelea kupata chanjo hiyo, kwa sababu haina madhara kwa mtoto anayenyonya au aliyetumboni.

Anasema Shirika la Afya Duniani (WHO), limethibitisha hakuna madhara, hivyo ni muhimu makundi hayo ya wanawake kujitokeza kupata kinga, kwa ajili ya usalama wao na watoto wao.

Anahimiza wanawake wanaonyonyesha kuendelea kutoa huduma ya kunyonyesha watoto wao mara baada ya kuchanja.

"Hata kama wana maambukizi ni vyema wakaendelea kunyonyesha hamna madhara yoyote kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto," anasema Dk. Grace.

Kwa mujibu wa taarifa ya mwisho iliyotolewa na Wizara ya Afya, hadi sasa Tanzania ina wagonjwa 858 wa UVIKO -19, huku vifo vikiwa ni 29.

TEKNOLOJIA

NA REUBENI LUMBAGALA, DODOMA

# Vituo vya umahiri viing'arishe Tanzania visiishie kuwa hadithi

MOJA ya mikakati ya kuipa sura mpya elimu kwa vitendo na kuongeza ufanisi kwa wahitimu vyuoni ni uwepo wa vituo vingi vya umahiri (centres of excellence) katika taasisi mbalimbali za elimu.

Dhamira hii ya ujenzi wa vituo vya umahiri ni mkakati wa wizara kutimiza wajibu wake wa msingi wa kuandaa na kuzalisha rasilimali watu wenye ujuzi wa kutosha, ili kusaidia utoaji wa huduma na uzalishaji bidhaa bora ili kulisha masoko ya ndani na nje ya nchi kwa maendeleo endelevu.

Kwa kuanzia, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia inatarajia kujenga vituo vinne vya umahiri katika Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (DIT) kampasi ya Mwanza.

Aidha, kingine ni ujenzi wa kituo cha umahiri katika sekta ya anga ambacho kitajengwa katika Chuo cha Usafirishaji (NIT) jijini Dar es Salaam , kwa upande wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA), kituo cha umahiri kinajengwa DIT kampasi ya Dar es Salaam na kwa upande wa nishati jadidifu kitakachojengwa DIT kampasi ya Arusha.

Taasisi hizo za umahiri zimejikijita kutoa elimu ya mafunzo ya ufundi kwa vitendo na weledi ili kuwa na raslimaliwatu wenye ujuzi, maarifa na stadi za kutosha badala ya kubaki kuwa wasomi wenye elimu ya nadharia pekee ambayo haina tija katika dunia ya sasa ya sayansi na teknolojia.

Ni kwa matarajio hayo basi, ujenzi wa nyumba za umahiri ni kielelezo kuwa kuna nia ya serikali ya kuandaa wahitimu wenye elimu inayoendana na mahitaji ya sasa katika soko la ajira iwe kujiajiri au kuajiriwa.

Akiwa katika ziara ya kutembelea Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam kampasi ya Mwanza, Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Omary Kipanga, anasema serikali inatarajia kutumia zaidi ya Shilingi bilioni 170 kujenga vituo vinne vya umahiri katika mikoa mine na kutangaza kuwa DIT kampasi ya Mwanza imetengewa Shilingi bilioni 37 kwa ajili ya kuwa na mafundi mahiri kuinua sekta ya ngozi.

Waziri Kipanga anaisema: "Tunataka ifikapo mwaka 2024 tuwe tumekamilisha ujenzi wa kituo cha umahiri katika msuala ya ngozi, ili sasa tuweze kuzalisha vijana ambao wakimaliza mafunzo waweze kuajiriwa au kujiajiri kwa kuzalisha bidhaa mbalimbali zitokanazo a malighafi hiyo inayopatikana kwa kiasi kikubwa nchini."

Pamoja na kwamba Tanzania ni nchi yenye idadi kubwa ya mifugo,



Viatu ni bidhaa ambazo zitaboreshwa kupitia kituo cha umahiri Mwanza kitakachotoa mafunzo ya sekta ya ngozi. **PICHA MTANDAO.**

> Naibu Waziri Kipanga, anavyosema: "Kimsingi serikali imeamua kwa dhati kuzalisha wanafunzi wenye ujuzi na umahiri, ambao utaleta tija kwenye Tanzania ya viwanda, hivyo inakwenda kujenga vituo vinne vya umahiri hadi kufikia mwaka 2024, ambacho ni kipindi cha miaka mitatu kuanzia sasa."

lakini kumekuwa na tija ndogo katika sekta hiyo. Ni kutokana na kuchelewa kuwepo kwa mikakati thabiti ya kuhakikisha mifugo inachangia kikamilifu kwenye pato la nchi na kukuza ajira kupitia mnyororo wa thamani wa sekta ya mifugo.

Hivyo, mkakati wa ujenzi wa kituo cha umahiri cha kuchakata ngozi, unaleta matumaini kwa wafugaji na wafanyabiashara kuhusu uwepo wa soko la uhakika wa bidhaa ya ngozi.

Aidha, kituo cha umahiri cha kuchakata ngozi kinaleta fursa ya ajira kwa vijana watakaopata elimu katika eneo hilo. Uwepo wa kituo cha umahiri cha kuchakata ngozi katika chuo cha DIT kampasi ya Mwanza, kunatoa fursa kwa wafugaji wa ng'ombe, kondoo, farasi na mbuzi kufuga mifugo yao kisasa, ili kuweza kupata bidhaa bora ya ngozi inayokidhi soko.

Kadhalika Watanzania watgemee kuanza kutumia bidhaa za ngozi halisi kama vile viatu, mikanda, pochi, mabegi na foronya za viti ambazo zitakuwa imara na zenye kudumu muda mrefu.

Kiujumla, ujenzi wa vituo vya umahiri ni mwendelezo wa mikakati ya serikali ya kuhakikisha taifa linazidi kusonga mbele kiuchumi na kiviwanda, ili kuongeza pato la wafugaji, wafanyabiashara , wawekezaji na taifa.

Naibu Waziri Kipanga, anavyosema: "Kimsingi serikali imeamua kwa dhati kuzalisha wanafunzi wenye ujuzi na umahiri, ambao utaleta tija kwenye Tanzania ya viwanda, hivyo inakwenda kujenga vituo vinne vya umahiri hadi kufikia mwaka 2024, ambacho ni kipindi cha miaka mitatu kuanzia sasa."

Vile vile, sekta ya anga ni eneo muhimu katika kukuza maendeleo na uchumi. Ujenzi wa kituo cha umahiri cha wanaanga katika Chuo cha Usafirishaji (NIT) unakusudiwa kupunguza gharama pengine kubwa za kufanya matengenezo ya ndege za Tanzania ughaibuni.

Hilo litafanikiwa kutokana na chuo kuzalisha wataalamu wa ndani, ambao watasaidia kufanya matengenezo madogo na makubwa kwa ndege hizo na kuokoa fedha nyingi, ambazo zingetumiwa kwa kuwatumia wataalamu kutoka nje ya nchi.

Ujenzi wa kituo cha umahiri kwa ajili ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano -TEHAMA unachangia kasi ya maendeleo nchini, ndiyo maana hata kaulimbiu ya Mbio za Mwenge wa

Uhuru kwa mwaka 2021, inasema "TEHAMA ni msingi wa taifa endelevu itumika kwa usahihi na uwajibikaji". Hii inatokana na ukweli kuwa serikali imeweka mifumo ya kuitumia katika shughuli nyingi za kiserikali, hali inayoongeza mahitaji ya wataalamu wa nyanja hiyo.

Aidha, ujenzi wa kituo cha umahiri cha nishati jadidifu au mbadala ni ufunguo wa kuongeza kasi ya ukuaji ya uchumi na maendeleo kutokana na upatikanaji wa nishati ya uhakika kwa wananchi na katika zama hizi za ongezeko la joto duniani na uharibifu wa mazingira unaokausha maji, lakini joto linalochangiwa na moshi kwenye injini za magari na nishati mbaya.

Reubeni Lumbagala ni Mwalimu wa Mlali Sekondari katika Wilaya ya Kongwa mkoani

**Dodoma.**

**Maoni: 0620-800462.**

ELIMU

NA ANI JOZENI

# NIDA ni maji ya shingo vitambulisho vya utaifa

## Asante NEC vya wapigakura ndivyo mkombozi



Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Dk. Faustine Ndugulile.

SUALA la kuwapo utambulisho wa taifa usio na utata lilitegemewa kumalizika baada ya kuanzishwa mradi wa vitambulisho vya taifa na kuundwa kwa Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA), kabla ya uchaguzi mkuu wa 2015.

Licha ya kuwa muongo mmoja unakaribia kukamilika tangu wakati huo kwani sasa ni miaka nane, bado idadi ya vitambulisho hivyo vilivyotolewa kwa Watanzania inahesabika.

Na hivi karibuni Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari wa Tanzania Dk. Faustine Ndugulile, anasema kadi za simu zaidi ya milioni 10, hazina namba za NIDA.

Ukilinganisha na vitambulisho vya wapiga kura unatambua kuwa kadi za mpiga kura kila mtu aliyejisajili alipata, tena papo kwa papo.

Inakuwa vigumu kuamini kama iliwezekana kwa vitambulisho vya kura ni kwanini juhudi zisifanyike kwenye vya NIDA, ili kila mmoja awe na utambulisho huo muhimu.

> Tofauti na hali hiyo, mwaka 2015 wakati wa kuandikisha kupiga kura, watu walijaza fomu, wakakaa kwa muda mfupi kusubiri kitambulisho kuandaliwa na baada ya dakika 30 picha zilikuwa zimepigwa zimesafishwa na 'data' muhimu zikawa zimewekwa humo na kuondoka na kadi zao.

Kwa kiasi kikubwa vitambulisho vya mpiga kura vilivyotolewa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), vimekuwa mbadala kwa vile vinatumiwa kujisali wateja, ili kufungua akaunti benki, kupata mafao pengine baada ya kukosa kazi na sasa kwenye chanjo ya COVID-19.

Kinachoonekana ni kuwa wenye dhamana au ofisi katika ngazi au ofisi za NIDA huenda hawajafanya juhudi za kukamilisha uandikishaji na utoaji wa namba pamoja na kadi, ili kukamilisha kazi hiyo. Inavyoelekea wanachukua muda wanajivuta huku watu wakihangaika kupata huduma hiyo, hivyo NIDA lazima idhihirishe mwaka hadi mwingine kuwa imetoa idadi kadhaa ya vitambulisho na kikitimia kiwango hicho huenda inatosha kuwekewa bajeti mwaka mwingine.

Kwa njia hiyo inaweza kufika mwaka 2025 Watanzania wakaendelea tena kutumia vitambulisho vya kura vya mwaka 2015, au leseni za udereva na hata pasi za kusafiria .

Tofauti na hali hiyo, mwaka 2015 wakati wa kuandikisha kupiga kura, watu walijaza fomu, wakakaa kwa muda mfupi kusubiri kitambulisho kuandaliwa na baada ya dakika 30 picha zilikuwa zimepigwa zimesafishwa na 'data' muhimu zikawa zimewekwa humo na kuondoka na kadi zao.

Ni zoezi la nusu saa, lakini NIDA hawajaweza kufanya jambo hilo hata kwa kuiga au kuita wataalamu kutoka Tume ya Taifa ya Uchaguzi NEC, na huu ni mwaka wa nane bado hawajakamilisha jukumu walilopewa.

Pengine watu wanajiuliza kama mradi huo unahitajika au unasubiriwa uamuzi kuwa wananchi wabaki na vitambulisho vya kura au pasi za kusafiria na leseni za udereva.

Watu wanajiuliza au kutaka kujua kuna tofauti na kazi ngumu katika kuandaa vitambulisho, hivyo maana imekuwa ni kazi ngumu na inayochukua muda mrefu kukamilika na watu kupata vitambulisho. Pengine tofauti na vya kura, kuna nini cha zaidi kwenye utambulisho wa NIDA?

Ila kuna eneo moja ambalo inaonekana namba za NIDA zimefanya kazi nzuri, kwa mfano kutumiwa kusajili simu na kuwezesha mawasiliano ya kufuatilia wahalifu, kwa vile kupeleleza simu imetoka kwa nani na ameandikishwa nani si jambo jipya, inawezekana uwepo wa namba za NIDA umerahisisha kiasi fulani ufuatiliaji.

Huenda ingekuwa tatizo kwa polisi kufuatilia mawasiliano ya watu wanaotumia simu, ambazo hazina mfumo wa pamoja wa utambulisho wa mhusika.

Kwa upande huo ni wazi kuwa yapo matokeo, ila ni ya matunda ya ziada ya mkakati wa utambulisho, ambao kimsingi unaelekea kukwama.

Eneo jingine ambapo mkakati huo hauwezi kukwama ila kuna uwezekano unasuasua ni utambulisho wa walipa kodi, hasa wanaoanza biashara na kuhitaji kutoa namba za NIDA, ili kupata kitamhulisho cha mlipa kodi (TIN). Zipo taasisi nyingine mbali na Mamlaka ya Mapato (TRA) ambazo zinawasilisha hesabu za kodi kwa TRA ambazo zinahitaji wale wanaolipwa kwa kutoa huduma kwao wawe na vitambulisho vya uandikishwaji kama mlipa kodi kutoka TRA, na mara nyingi inakuwa vigumu kupata utambulisho huo haraka.

Ila inawezekana tatizo siyo kubwa kwani kati ya simu milioni 10 ambazo hazina vitabulisho au namba za NIDA, wengi zaidi watakuwa wale ambao hawana msukumo wa kutosha kibiashara unaowalazimisha kuwa nazo.

Kwa maana hiyo kasi ya kufanyakazi NIDA ina umuhimu, ili kupata vitambulisho pamoja na namba hizo katika masuala ya uandikishaji kadi za simu na halafu ulipaji kodi, kwani maeneo kama TRA ni muhimu, kwani ndiyo yanayohakikisha kuwa taasisi hiyo itaendelea kuwapoa . Hata hivyo vitambulisho na namba ni vya lazima katika taratibu za kiserikali kwa mfano ndizo zinazotumiwa kusajili watu mathalani kwenye chanjo za COVID-19.

Pengine taratibu na namna yake ya kujumuisha kutambuliwa kwa raia au mkazi ni ya kina zaidi kuliko utambulisho mwingine uliopo hata ungekuwa ni pasi ya kusafiria ya mpiga kura, inayokaribiana na ile ya NIDA kwa umaarufu, kabla ya pasi ya kusafiria ambayo haimilikiwi na watu wengi wa kawaida. Inawezekana mradi huo umegharimu pesa nyingi kuliko ilivyotakiwa, ukilinganisha na zile zinazotumiwa na NEC inayotengeneza vitambulisho haraka tena papo kwa papo.

Pengine ingekuwa rahisi kwa NIDA kutoa namba za utambulisho katika Wilaya mbalimbali halafu zitumike kutoa vitambulisho kwa kasi zaidi kwa kushirikiana na mamlaka nyingine, ili kuharakisha upatikanaji wa kadi hizo muhimu.





# Taasisi yaelimisha vijana athari mimba za utotoni

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

TAASISI ya Maendeleo ya Vijana Dodoma (DOYODO), imetoa mafunzo ya afya ya uzazi na madhara ya mimba za utotoni kwa vijana zaidi ya 1,250 jijini Dodoma.

Mkurugenzi wa Doyodo, Rajabu Nhunga, alisema hayo wakati alipozungumza na waandishi wa habari kuhusu mafanikio ya mradi wa kukabiliana na mimba za utotoni ulioanza tangu mwaka 2019.

Nhunga alisema mradi huo unalenga kupunguza mimba za utotoni kwa kuboresha huduma rafiki kwa vijana za afya ya uzazi na kuwajengea stadi za maisha.

Alisema mradi huo unatekelezwa kwa miaka mitatu kuanzia 2019 mpaka 2021 na unajulikana kwa jina la 'magauni manne girls empowerment project' na unatekelezwa kwa ufadhili wa Shirika la Kimataifa la DSW-Tanzania. Alibainisha kuwa idadi hiyo ni wale ambao wamejengewa uwezo moja kwa moja na Doyodo lakini baada ya mafunzo hayo na wao wamekuwa na jukumu la kuwaelimisha vijana wenzao kwenye maeneo yao.

Alizitaja baadhi ya kata ambazo taasisi hiyo inafanya kazi na makundi hayo ya rika la vijana hao kuwa ni Mnadani, Nzuguni, Miyuji na Chang'ombe.

Aliongeza kuwa nje ya vijana hao pia walifanikiwa kuunda klabu za vijana kwenye kata hizo ambazo mradi unatekelezwa na vijana 150 wamejengewa uwezo na kati yao vijana 25 wanashiriki katika vikao vya maendeleo kwenye kata zao.

Aidha, alisema Doyodo imefanikiwa kuwajengea uwezo wanafunzi na walimu kwenye shule 10 za jijini hapa kwa kuwafikia wanafunzi wasiopungua 250 katika shule hizo ambapo sekondari zipo tano na msingi tano.

Kadhalika, alisema taasisi imefanikiwa kuwakutanisha baadhi ya vijana wengine na wadau wa afya ya uzazi kutoka Mikoa ya Dar es Salaam, Arusha, Shinyanga na Mwanza kwa lengo la kujifunza mbinu mpya za kupunguza mimba katika umri mdogo.

Alifafanua kuwa katika kuhakikisha wanafanikiwa kwenye mpango huo wamekuwa wakiwatumia wataalamu wa afya kutoka Wizara ya Afya na baadhi ya vijana wenye elimu hiyo ya mambo ya elimu ya uzazi.

Aliyataja baadhi ya malengo ni kuendelea na mapambano ya mimba za utotoni kwa kuwafikia vijana wengine zaidi kwenye kata 37 za Dodoma Mjini na wilaya 6 za Mkoa wa Dodoma na hata nje ya mkoa huo.

Mkurungenzi huyo alisema tatizo la ufinyu wa rasilimali fedha ndio limekuwa likisababisha kushindwa kuwafikia moja kwa moja vijana hao kutoka maeneo yote.




Mjasiriamali Rachel Francis (kushoto), akimwonyesha mteja bidhaa kwenye maonyesho ya wajasiriamali ya Nanenane yanayoendelea viwanja vya Nyerere Square jijini Dodoma jana. **PICHA IBRAHIM JOSEPH**

# Washauriwa matumizi miamala mbadala

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WATANZANIA wamehamasishwa kutumia huduma mbadala za miamala ya CRDB ili kujiepusha na misongamano isiyo ya lazima katika kukabiliana na maambukizo ya corona.

Rai hiyo ilitolewa jana na Meneja wa CRDB Kanda ya Kati, Chabu Miswaro, katika hafla ya kukabidhi gari aina ya Toyota IST kwa mshindi wa pili wa kampeni ya 'SimBanking Mzigo Promosheni' Madina Ramadhani.

Alisema ni vyema Watanzania wakafanya miamala ya fedha kwa kutumia SimBanking kwa kuwa ni njia mbadala inayoshauriwa hivi sasa kutokana na hali ilivyo.

Awali, akitoa maelezo kuhusu promosheni hiyo, Mkuu wa Kitengo cha Wateja Binafsi, Stephen Adili, alisema mshindi huyo ni mfanyakazi wa kituo cha mafuta kilichopo Kisasa jijini Dodoma na amejishindia gari hilo kwa kufanya miamala mingi zaidi kupitia huduma ya SimBanking.

Alibainisha kuwa kampeni hiyo inalenga kuwahamasisha wateja kuwa na utamaduni wa kutumia mifumo ya kidijitali ikiwamo SimBanking kufanya miamala yao.

"Huyu mshindi aliyeshinda leo ameshinda kwa kufanya miamala ya kawaida kabisa kama kununua vocha, umeme, kuhamisha fedha, mbali na kuwa na mshindi wa gari pia kwenye kampeni hii kila siku kuna washindi wa tatu wa Sh.100,000,kuna washindi wengine 13 kila siku wanashinda 30,000," alisema.

Alisema kiasi cha Sh. milioni 800 kimetengwa kwa ajili ya kutoa zawadi kwa washindi wa kampeni hiyo huku akisema asilimia 90 ya miamala ya SimBanking ni bure.

Kwa upande wake, mshindi wa gari hilo, Madina Ramadhani, alisema alikuwa akifanya miamala ambayo hajaamini kama ingemwezesha kuwa mshindi wa gari hilo.

"Mimi nafanya kazi ya kujaza mafuta Sheli ya Kisasa na mshahara wangu ni Sh. 200,000 lakini hii hii nilikuwa naitumia kufanya matumizi mbalimbali kwa SimBanking imeniwezesha leo kuwa mshindi," alisema.

# Askofu ataka maombi corona

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

ASKOFU wa Kanisa la Endtime Harvest, Dk. Eliah Mauza, amemwomba Rais Samia Suluhu Hassan kutangaza siku maalum ya maombi ya ugonjwa wa corona.

Akizungumza juzi kwenye ibada, Askofu huyo alisema serikali na viongozi wa dini wanapaswa kuendelea na maombi ya kuombea ugonjwa huo kama walivyofanya awali ili Mungu atoe uponyaji kupitia chanjo ya UVIKO-19 inayotolewa.

"Naomba serikali itangaze maombi ya siku kadhaa kwa wananchi, kila mmoja kwa imani yake aombe tuweze kushindana na ugonjwa wa UVIKO-19," alisema.

Alisema wanadamu wanapaswa kuendeleza huduma ya maombi ili kushindana na shetani ambaye anataka kuiangamiza dunia kupitia ugonjwa huo.

"Tunaomba serikali itangaze siku kadhaa za maombi ili kila mmoja ajumuike kumuomba Mungu ili kuepukana na ugonjwa huu na magonjwa mengine hatarishi," alisema.

Aliongeza: "Sote tukielekeza nia zetu katika maombi pamoja na chanjo hii inayotolewa kwa wananchi basi jamii itakuwa salama kutokana na kwamba wanaomba, lakini pia wanaendelea kupata chanjo kutoka kwa wataalamu wa afya kama inavyoelekezwa."

Hata hivyo, alikemea jamii kuondoa hofu na upotoshaji kwenye mitandao ya kijamii kuhusu chanjo hiyo.

"Ni vyema wataalamu wa afya waendelee kuwapa elimu wananchi ili waweze kuchoma chanjo hiyo ya kujikinga na ugonjwa wa corona," alisema.

Alisema wao kama viongozi wa dini wanaendelea kutoa elimu kwa jamii kuhusiana na kupata chanjo ambayo itawasaidia kujikinga na ugonjwa huo hatari unaoitesa dunia.

Alimpongeza Rais Samia kwa utendaji kazi wake unaolenga kuinua uchumi wa nchi.

"Rais Samia anastaili pongezi kutokana na miradi mbalimbali ya maendeleo hapa nchini kuendelea kutekelezwa ili wananchi waweze kunufaika nayo," alisema.

**Aliongeza: "Sote tukielekeza nia zetu katika maombi pamoja na chanjo hii inayotolewa kwa wananchi basi jamii itakuwa salama kutokana na kwamba wanaomba, lakini pia wanaendelea kupata chanjo kutoka kwa wataalamu wa afya kama inavyoelekezwa."**



# Mbaroni madai kusafirisha magunia 34 ya tumbaku

**Na Grace Mwakalinga,** CHNYA

WATU wawili wanashikiliwa na dola mkoani Mbeya kwa tuhuma za kusafirisha shehena ya magunia 34 ya tumbaku kwa njia ya magendo kuelekea katika nchi jirani ya Malawi. Watuhumiwa walikamatwa juzi kwenye kizuizi cha barabarani katika mji mdogo wa Makongorosi, wilayani Chunya wakisafirisha tumbaku hiyo kwa kutumia lori.

Akizungumzia tukio hilo, Mkuu wa Wilaya ya Chunya, Mayeka Simon, alisema waliokamatwa ni wakulima wa zao hilo ambao walikuwa wanasafirisha kwa njia za panya ili wakauze nchini humo.

Alisema watu hao walipofika kwenye kizuizi cha Makongolosi, askari walisimamisha gari hilo na kulipekua na kubaini magunia hayo yenye tumbaku na kuyakamata.

Alisema kutokana na tabia ya utoroshaji wa zao la tumbaku kuathiri wakulima waliojiunga na vyama vya ushirika, na pato la nchi kwa kukwepa ushuru, Kamati yake ya Ulinzi na Usalama iliamua kuweka vizuizi kuzuia utoroshaji huo.

"Hii ni mara ya pili katika msimu huu wa mauzo ya tumbaku tunafanikiwa kukamata marobota yakitoroshwa kwenda nchi jirani ya Malawi, tunazuia biashara hii ya magendo kwa sababu ina athari kubwa kwa wakulima wetu na pia inasababisha pato la serikali kupotea," alisema Mayeka.

Akifafanua alisema wakulima wa tumbaku wilayani Chunya wanalima zao hilo kwa mkataba kupitia vyama vya ushirika na wanakopeshwa pembejeo zote na wanunuzi na hutakiwa kulipa deni hilo wakati wa kuuza tumbaku yao.

Alisema kwa mantiki hiyo tumbaku yote hutakiwa kuuzwa kupitia vyama vya ushirika ambako madeni ya wakulima hukatwa na serikali nayo hukusanya ushuru na kodi yake kirahisi kwenye vyama hivyo vya ushirika.

"Inapotokea mkulima ambaye alikopeshwa pembejeo hauzi mazao yake kwenye ushirika, huwalazimu wakulima wenzake kumlipia deni lake la pembejeo kwa vile walikopeshwa pamoja, lakini sisi kama serikali tunakosa kodi na ushuru wa halmashauri, ndio maana tuliamua kudhibiti biashara hii ya magendo," alisema Mayeka.

Naye Kaimu Meneja wa Chama Kikuu cha Ushirika wa Wakulima wa Tumbaku wilayani Chunya (CHUTCU), Daniel Mpigasupi, alisema wakulima hao wamefanya kosa kwa mujibu wa sheria ya vyama vya ushirika na kwamba watachukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria hiyo.

Aliwaonya wakulima wengine ambao wamepanga kusafirisha tumbaku kwenda kuuza maeneo mengine nje ya utaratibu kwa ushirika akidai wanaweza kupata hasara kwa vile hata huko wanakopeleka wanauiza kwa bei ndogo ikilinganishwa na ile ya kwenye ushirika.

Mkuu wa Idara ya Kilimo, wilayani humo, George Mwinuka, alisema serikali inaendelea kutengeneza mazingira rafiki kwa wakulima na kwamba kutumia njia za panya kuuza mazao yao kunawakosesha fursa ya kuuza kwa bei elekezi.



Wanafunzi wa Taasisi ya Teknolojia ya Ujenzi Mbeya (ICot) wakiendelea na ujenzi wa barabara katika Kata ya Kajunjumele kuelekea katika mwalo wa Kafyofyo iliyoko Wilaya ya Kyela mkoani Mbeya juzi. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Ukosefu wa utaalamu wakwamisha upangaji bajeti

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

WAFANYABIASHARA na wajasiriamali wengi nchini wanashindwa kufikia malengo ya shughuli zao kutokana na kutokuwa na utaalamu wa namna bora ya upangaji wa bajeti kuanzia ngazi ya familia.

Kukosa elimu ya upangaji bajeti kwa makundi hayo kumechangia kukwamisha ukuaji wa biashara na kushindwa kufikia malengo na kuendelea kulimbikiza madeni na kusababisha msongo wa mawazo.

Mkurugenzi wa Shirika la Elimisha, Festo Sikagonamo, alisema lengo la kuanzishwa kwa shirika hilo ni uwezeshaji vijana na wanawake wasiokuwa na ajira kwa kuwafundisha mbinu za kupata kazi halali zinazolenga kutatua tatizo ili kuwa na maisha bora endelevu na yenye kutimiza ndoto zao kuanzia ngazi ya kaya.

Kutokana na vikwazo mbalimbali vinavyosababishwa na ukosefu wa elimu ya upangaji bajeti kuanzia ngazi ya familia Sikagonamo ameanzisha programu ya kuwajengea uwezo wajasiriamali na wafanyabiashara wanawake na vijana umuhimu wa bajeti.

"Tulifanya utafiti tukabaini kuwa wananchi hawana uelewa juu ya masuala ya upangaji wa bajeti hivyo kushindwa kutimiza malengo yao kwani hawana matumizi mazuri ya fedha, tumeiona mwitiko wa wananchi hususani wajasiriamali baada ya kupewa elimu hiyo kuona mabadiliko," alisema Sikagonamo.

Alisema hadi sasa wafanyabiashara na wajasiriamali zaidi ya 100 wa jijini Mbeya, wamepatiwa elimu ya upangaji bajeti kuanzia ngazi ya familia na kwamba hata taasisi na mashirika ya umma na binafsi wamepatiwa elimu hiyo.

Aliongeza kuwa pia wamepatiwa elimu ya uongozi kwa wanawake na wanaume ikilenga zaidi kuwahamasisha kugombea kwenye kamati mbalimbali za uongozi wa mtaa au vijiji ambako huko wataweza kuwasilisha kero zao na kutatuliwa.

Mtendaji wa Kata ya Sinde, Hawa Kajula, ambaye alitoa mafunzo ya uongozi kwa wajasiriamali hao, aliwahamasisha kujitokeza kugombea nafasi mbalimbali za kamati ili kupaza sauti zao.

Alisema uongozi bora unaanza kutengenezwa kuanzia ngazi ya chini kwenye mitaa na vijiji na kwamba akiwaandalia vyema anaweza kuja kiongozi mzuri hapo baadaye.

Baadhi ya wanufaika wa mafunzo hayo, akiwamo Regina Sanga, alisema kuwa upangaji wa bajeti kuanzia ngazi ya familia ni jambo muhimu katika mafanikio ya nchi na kwa mtu mmoja mmoja.

Sanga ambaye ni mkulima wa mboga na matunda alisema laiti elimu ya upangaji bajeti angeipata tangu zamani angekuwa mbali kimaendeleo, amekuwa hana bajeti na fedha anayoipata kutokana na biashara ya kuuza mboga, lakini kwa sasa atahakikisha anazingatia nidhamu ya matumizi ya fedha anayoipata.

# Dk. Tulia atoa mil. 500/- kujenga kituo cha afya

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

MBUNGE wa Jimbo la Mbeya Mjini ambaye pia ni Naibu Spika wa Bunge la Tanzania, Dk. Tulia Ackson, ametoa Sh. milioni 500 kwa ajili ya ujenzi Kituo cha Afya cha Iyela ili kuwasaidia wananchi kukabiliana na adha ya kutembea umbali mrefu na gharama kupata matibabu maeneo mengine.

Alitoa msaada huo jana wakati akizungumza kwenye mkutano maalumu na wananchi wa Iyela uliokuwa na lengo la kuwaeleza vipaumbele vilivyowekwa na serikali katika kuwasaidia wananchi.

Alisema katika bajeti ya mwaka 2021/2022 serikali imejikita kuboresha miundombinu ya barabara elimu na afya.

Kwa kutambua umuhimu huo, Dk. Tulia alisema serikali imetoa kiasi cha Sh. milioni 500 kuanza ujenzi wa kituo hicho ambacho kitakuwa msaada mkubwa wa wananchi wanaozunguka eneo hilo huku akiwaeleza kuhusu uamuzi aliofanya kwa kushirikiana na Halmashauri ya Jiji ya kuanza mara moja ujenzi wa kituo hicho.

"Kwa muda mrefu wananchi wa Kata ya Iyela, wamekuwa wakipata huduma za matibabu maeneo mengine kwa kutambua adha hiyo serikali imetoa kiasi cha Sh. milioni 500 kuanza ujenzi huku tukiwahamasisha pia wananchi kushiriki nguvu kazi zao kituo hiki kikamilike kwa wakati," alisema Dk. Tulia.

Katika hatua nyingine, Dk. Tulia alifanya ziara ya kuwatembelea baadhi ya wananchi hususani wenye mahitaji maalumu akiwamo Joyce Isack, mkazi wa Sinde, ambaye alipata ajali ya gari na kumsababishia ulemavu wa maisha.

Alimsaidia mifuko 50 ya saruji kwa ajili ya kumuwezesha kukamilisha ujenzi wa nyumba yake, vilevile alimsaidia Gabriel Mwangobola, mkazi wa Uyole baiskeli mwendo kwa ajili ya kutembelea baada ya kupata ajali miaka kadhaa iliyopita akiwa mwalimu wa Shule ya Sekondari Sangu pamoja na Sh. 600,000 ili kuanzisha biashara itakayomsaidia kujikwamua kiuchumi.

Baadhi ya wananchi wa Iyela akiwamo Tukupasya Wisdom, alisema kujengwa kwa kituo hicho kutasaidia wajawazito kupata huduma karibu ikilinganishwa na ilivyokuwa awali walienda kujifungua maeneo ya mbali.

Wisdom alisema kulingana na miundombinu ya eneo hilo walilazimika wajawazito kubebwa kwenye pikipiki kwenda maeneo mengine kama Kituo cha Afya cha Nzovwe kujifungua.





# WanaCCM walia kupanda bei ya bidhaa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

VIONGOZI na wanachama wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Mjini Magharib Unguja, wameiomba serikali kulipatia ufumbuzi tatizo la kupanda bei za bidhaa ili kuwaondolea mzigo wananchi wa kipato cha chini.

Rai hiyo ilitolewa jana na viongozi na wanachama wa chama hicho katika kikao maalum na Mjumbe wa Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya CCM Taifa, Hemed Suleiman Abdulla, kilichofanyika katika ofisi za CCM Amani Zanzibar.

Asha Salumu, mmoja wa wanachama hao, alisema hali ya sasa kwa bidhaa hasa za chakula hairidhishi, hali ambayo imewaumiza wananchi, akitolea mfano kupanda bei ya mkate na mafuta ya kula.

Akitoa ufafanuzi juu ya hoja hizo Mjumbe wa Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya CCM Taifa, Hemed Suleiman Abdulla, alisema kuwa serikali imeshatoa maelekezo kwa wizara husika kupanga namna bora ya bei za bidhaa ili zisiwaumize wananchi. Hemed ambaye ni Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, alisema serikali haitomvumilia mfanyabiashara yeyote atakayekwenda kinyume cha bei elekezi zinazotolewa na serikali na akiwathibitishia kuwachukulia hatua wafanyabiashara wanaokiuka maelekezo ya serikali.

Akigusia suala la uongozi ndani ya chama, Hemed aliseam CCM ina taratibu zake za kikatiba za kuwapata viongozi, huku akiwataka wanachama kuwa wavumilivu na kusubiri muda wa uchaguzi wa ndani ya chama na kuacha tabia ya kupanga safu.

Kuhusu tatizo la dawa za kulevya, aliwaomba viongozi hao kuunga mkono jitihada zinazochukuliwa na serikali kuu katika kupambana na kadhia hiyo ili kujenga taifa lenye afya bora na kupata viongozi bora wa baadaye.

Alieleza kuwa, serikali itachukua hatua kali ikiwamo kufanya marekebisho ya baadhi ya sheria kwa lengo la kuwadhibiti wanaojihusisha na vitendo haramu vya kuharibu jamii ya Wazanzibari.

Aidha, alitaka jamii kurudi katika jukumu lao la msingi la kusimamia malezi bora kwa vijana wao ili kuwaepusha dhidi ya vitendo viovu vilivyokithiri katika jamii.

Katika kikao hicho Hemed aliwataka viongozi wa majimbo kuepukana na majungu na fitina badala yake wafanye kazi kwa kushirikiana kwa kuwashirikisha vingozi wa serikali na chama katika ngazi zote wakati wakitekeleza majukumu yao.

Pia aliwataka viongozi hao kuwa mstari wa mbele katika kushawishi jamii ili kuendelea kujiunga na CCM kwa lengo la kuongeza idadi ya wanachama ikiwa ni miongoni mwa jitihada za kukijenga chama.

Naye Katibu wa CCM Mkoa wa Mjini, Abdallah Mwinyi, alisema kuwa mkoa huo unasimamia vyema utekelezaji wa ilani hadi sasa, ambapo viongozi wa majimbo wapo karibu na wananchi kutatua kero zinazowakabili.

Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Mjini, Talib Ali, alisema katika uchaguzi Mkuu wa Oktoba 2020 kwa mara ya kwanza mkoa huo kuchukua ushindi wa majimbo yote kwa nafasi zilizogombewa.



Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud (wapili kulia), akisalimiana na viongozi wa Chama cha ACT-Wazalendo baada ya kuwasili kisiwani Pemba kwa ziara za kichama na serikali katika Uwanja wa Ndege Pemba. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mjini Magharibi yajinadi utekelezaji miradi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MKUU wa Mkoa wa Mjini Magharib Unguja, Idrissa Kitwana, amesema serikali imedhamiria kuimarisha miradi mbalimbali ya maendeleo na huduma za kijamii.

Miongoni mwa miradi ni barabara za ndani ili wananchi kufanya shughuli zao kwa urahisi katika kujipatia kipato.

Mustafa alieleza hayo wakati akizungumza na wananchi wa Shehia ya Mnarani, Pangawe na Mambosasa katika mwendelezo wa mikutano yake na wananchi wa kutatua kero zinazowakabili.

Alisema Serikali ya Zanzibar itaendelea kutekeleza ahadi zake kwa vitendo katika kuimarisha huduma katika nyanja tofauti ili kuharakisha kasi za maendeleo na kukuza uchumi wa mwananchi.

"Serikali inaendelea na mipango yake ya kuimarisha na kusogeza karibu huduma za kijamii kwa wananchi ili kuona wanaendelea kufaidi na fursa mbalimbali zinazotolewa na serikali yao katika sekta tofauti ikiwamo miundombinu ya barabara," alisema Kitwana.

Aidha, alisema Serikali ya Mkoa wa Mjini kupitia Mabaraza ya Manispaa ya Mkoa huo inakusudia kuzitumia kanuni na sheria ndogo za usafi ili kutoa adhabu ya papo kwa papo kwa watu watakaobainika wanatupa taka ovyo na kuchafua mji.

"Tayari kanuni zishafanyiwa mapitio kwa ajili ya kufanyiwa kazi kwa watu watakaochafua mazingira kwa ajili ya kuimarisha usafi wa maeneo yetu mtu atakayeonekana anatupa taka ovyo atatozwa faini," alisema Kitwana.

Baadhi ya wananchi wa maeneo hayo, walielezea kusikitishwa kwao na suala la uchafu uliopo katika shehia zao husussani utupati wa taka ovyo hasa za pempasi zilizotumika hatua ambayo imekuwa kero na kuchafua mazingira na inahatarisha usalama wa afya zao kwa kusababisha maradhi ya mlipuko.

"Mkuu wa Mkoa niulize hizi pempasi ni mradi wa viongozi, maana imekuwa kero katika shehia zetu, maeneo yote yamejaa pempasi zilizotumika, zikichomwa haziungui, zikifukiwa haziozi sasa... naomba zipatiwe ufumbuzi, tulipiga marufuku mifuko ya plastiki na tumeweza na hizi tuzuwie turudishe utamaduni wa zamani watoto wavalishwe nepi," alisema Idrissa Nahoza Issa.

Naye Mwakilishi wa Jimbo la Pangawe, Ali Suleiman Ali, alisema uongozi wa jimbo hilo umekuwa ukifanya kazi kwa karibu na serikali kutatua tatizo la maji ambapo imefanikiwa kupunguza kwa kiasi kikubwa tatizo.

# Sababu za kupaa kwa bei ya mafuta

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

BEI ya mafuta ya petroli, dizeli na mafuta ya taa imeendelea kuongezeka Zanzibar kwa mwezi Agosti mwaka huu, kutokana na sababu mbalimbali.

Miongoni mwa sababu hizo ni gharama za uingizaji wa bidhaa hiyo katika Bandari ya Dar es Salaam.

Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano kutoka Mamlaka ya Udhitibi wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar (ZURA), Mbarak Hassan Haji, akitangaza bei hizo zilizoanza kutumika jana, alisema bei ya mafuta ya petroli, dizeli na mafuta ya taa imepanda ukilinganisha na mwezi uliopita.

Aliyasema hayo wakati akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake Maisara Mjini Unguja, na kwamba petroli itauzwa kwa Sh. 2,379 kwa mwezi huu kutoka Sh. 2,327 mwezi uliopita.

Alisema dizeli itauzwa kwa Sh. 2,287 kwa mwezi huu kutoka Sh. 2,222 ya mwezi uliopita wakati kwa mafuta ya taa alisema bei ya rejareja itakuwa.

Alisema sababu zilizopelekea kupanda kwa bei ni kubadilika kwa wastani wa bei za uuzaji wa bidhaa hizo katika soko la dunia, thamani ya shilingi ya Tanzania kwa dola ya kimarekani, gharama za usafiri, bima na Premium hadi Zanzibar, kodi za serikali na kiwango cha faida kwa wauzaji wa jumla na rejareja.

Hata hivyo, alisema ZURA inapanga bei kwa kuzingatia wastani wa mwenendo wa mabadiliko ya bei za mafuta duniani kwa mwezi uliopita ili kupata kianzio cha kufanyika mabadiliko ya bei za mafuta kwa mwezi huu.

Pia alieleza kuwa licha ya kuwa bei ya mafuta kuongezeka, lakini yapo ya kutosha kwa matumizi ya Zanzibar.

Aliwaomba wananchi kuhakikisha kuwa bei zilizotangazwa ndio bei halali na kuwasisitiza kununua mafuta katika vituo vilivyokuwapo kihalali ili kuepuka kuuziwa mafuta ya magendo na kudai risiti.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 0782253676

**KATIKA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**DAR ES SALAAM**

**UTHIBITISHO WA USIMAMIZI WA MIRATHI**

**MIRATHI NA 77 YA MWAKA 2021**

**MAOMBI YA BARUA ZA USIMAMIZI WA MIRATHI YA MAREHEMU ASTERIA NICHOLAS MANYAKA**
**MWOMBAJI/WAOMBAJI**
**JERROLD GWASEKO**

**TAARIFA YA KAWAIDA**
**(kanuni ya 75)**

Watu wote wanaodai kuwa na haki ya marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia mashauri haya katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa uthibitisho wa barua za usimamizi wa mirathi kwa waombaji/mwombaji hapo juu Mapingamizi yoyote kuhusu haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 13 mwezi 9 mwaka 2021 Imewasilishwa dar es salaam ,leo tarehe 13 mwezi wa 7 2021

NAIBU MSAJILI

116398902

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ROBEL AYOB HAILE** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **TOYOTA MARK X** yenye namba za usajili **T 789 ATD** chasis namba **GRX1200041613** engine namba **4FRFSE0100992**,yeyote atakayeiokotab atoe taarifa kituo chochote cha polisi Polisi taarifa **DOD/DOD/ RB/339180/2021**

116399002

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika Mahakama ya Mwanzo**
**MJINI MOROGORO**
**Usimamizi wa Mirathi**
**NO.188/2021**

**Ombi la ROSE NICHOLAUS KEYAMBA Kuteuliwa Msimamizi wa Mirathi ya Marehemu NICHOLAUS KANUTI KEYAMBA**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaalikwa kuja kuhudhuria shaurini mnamo tarehe 14/07/2021 kabla huyo mwambaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo. Wosia wa marehemu huyo upo hapa mahakamani waweza kukaguliwa.
Tarehe 15/06/2021

HAKIMU
MOROGORO

116399102

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA.**

**KUITWA SHAURINI KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA MASWA SHAURI NAMBA 77 LA MWAKA 2020.**

**KESI YA MADAI YA ARDHI KATI YA BELE NSOMI (MWOMBAJI) DHIDI YA GITI NG'HABI (MJIBU MAOMBI)**

Giti Ng'habi kwa kuwa mwombaji hapo juu amefungua maombi dhidi yako katika baraza la ardhi na nyumba la wilaya ya Maswa kwenye shauri tajwa hapo juu, unatakiwa kuleta barazani utetezi wako wa maandishi kabla tarehe 30/8/2021.

Pia unajulishwa kuwa maombi haya yamepangwa kutajwa siku ya tarehe 30/8/2021 saa 2:30 asubuhi mbele ya mhe J.T.Kaare Mwenyekiti baraza la ardhi na nyumba Wilaya ya Maswa.

Unajulisha kwamba iwapo utakaidi kupokea wito huu au kupuuza bila udhuru na kushindwa kufika siku iliyopangwa ,Baraza litalazimika kusikiliza maombi hata upande mmoja na kutoa uamuzi dhidi yako.

Hati hii imetolewa kwa amri ya mwenyekiti wa Baraza la ardhi na nyumba la wilaya ya Maswa leo tarehe 29 mwezi wa saba mwaka 2021.

J.T.KAARE
MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W)
MASWA.

216399002

## KUPOTEA KWA PASIPOTI

**MUSSA MARUNGU MUSSA** anatangaza kupotelewa na pasipoti (hati)ya kusafiria yenye namba za usajili **TAE 249804** iliyotolewa na wizara ya mambo ya ndani ya nchini SWEDEN mwaka 2019, yeyote atakayeiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Polisi taarifa **DAR/OST/RB/388067/2021**

116399402

## KUPOTEA KWA PASIPOTI

**JOYCE CHARLES MTAWALI** anatangaza kupotelewa na pasipoti ya kusafiria (hati) yenye namba za usajili **TAE 249803** iliyotolewa na wizara ya mambo ya ndani nchini **SWEDEN** mwaka **2019**,yeyote atakayeiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi Polisi taarifa **DAR/OST/ RB/388064/2021**

116399502

## KUPOTEA KWA PASIPOTI

**ZAKIA ABDALLAH MHAVILLE** anatangaza kupotelewa na pasipoti ya kusafiria (hati) yenye namba za usajili **TAE 249802** iliyotolewa na wizara ya mambo ya ndani nchini SWEDEN mwaka 2019, yeyote atakayeiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Polisi taarifa **DAR/OST/RB/388062/2021**

116399602

**ABA AJA COMPANY LIMITED**
**TAARIFA/NOTISI**
**Katika mahakama ya mwanzo kizumbi**
**Iliyopo shinyanga**
**SHAURI LA MADAI NAMBA 26/2021**
**NEW DAMI &COMPANY-(MDAI)**
**NAYAZ NAZIM BHANJI-(MDAIWA)**
**KWA.NAYAZ NAZIM BHANJI**

Unataarifiwa kuwa nimepewa hati ya kukamata mali dhidi yako katika shauri la madai namba 26 ya 2021 ya mahakama ya mwanzo kizumbi iliyopo shinyanga.unataarifiwa kuwa ulipe sh.11,200,000/= kwa ajili ya mdai new Dami &Company ndani ya siku kumi nan ne(14) za kazi tangia siku ya kutolewa kwa taarifa (tangazo ) hii pamoja na gharama za ukazaji hukumu.usipotekeleza hatua nyingine za ukazaji hukumu zitaendelea dhidi yako bila taarifa/notisi nyingine kutolewa kwako.

C. R. Kabonga
Dalali wa Mahakama
SHINYANGA

116400302

## KUPOTELEWA NA VYETI



**NDG.ROBERT IPYANA ADAM**
Anatangaza kupotelewa na vyeti vifuatavyo :
1. Cheti kidato cha Nne(IV), na. **Cs 12 00225893,** chenye usajili na.s 1361-0169 cha mwaka 2021, katika shule ya sekondari Samora Machel-Mbeya,
2. Cheti cha Ordinary Diploma (NTA 6), chenye na.NTA 6 0006359, na usajili na.201341209, cha mwaka 2018, katika Chuo cha Mbeya University of Science & Technology (MUST),
3. Cheti cha Transcript na.13720
4. Cheti cha kuzaliwa.

Kwa yeyote atakayeviona anaombwa aripoti kituo chochote cha polisi.
TAARIFA YA POLISI : **MBE/MBE/RB/341786/2021 & MBE/MBE/RB/341785/2021**

116400402

## MNADA WA HADHARA

Kwa idhini tuliyopewa na **TUJIJENGE TANZANIA LTD, Sepco** tutauza kwa mnada wa hadhara Mali ya wadaiwa Sugu kama ilivyotangazwa gazetini

| Mdhamini /Mdaiwa | Dalali | Aina ya Mali /Mahali | Tarehe mnada |
|---|---|---|---|
| MARY HARRIETH CHIBIBI LONGWAY/ AMINA MARTIN BAGULE | **SEPCO** Debt Collection & Auctioneering Co. Ltd | Toyota land Cruiser T.297 ASV, Makumbusho Yard-Dar | 24.08.2021 |

Mnada utafanyika mahali dhamana ilipo kuanzia saa nne asubuhi. Mteja atalipa 25% siku ya mnada, 75% atalipa ndani ya siku 14 akishindwa kulipa 25% hairudishwi. Gharama za kubadili umiliki ni juu ya mnunuzi.

**Mawasiliano piga: -**
**SEPCO - 0715683777/0712670704**

116400902

## KUPOTEA KWA CHETI



**ALOYCE Z SOLOMONI** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye Index namba **S.2824-0025** kilichotolewa na Baraza la Mitihani kupitia **NDEKI SEKONDARI** mwaka **2016.**

Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi.Taarifa ya polisi: **MAN/BAB/ RB/356412/2021**

116400502

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku
Tupigie
0782253676

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji
THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Msumbiji, Rwanda zakomboa mji uliodhibitiwa na waasi

**Maputo,** MSUMBIJI

VIKOSI vya Msumbiji vikisaidiwa na wanajeshi wa Rwanda vimewafurusha wanamgambo wa itikadi kali, waliokuwa wanaudhibiti mji muhimu wa bandari wa Mocimboa da Praia eneo la Kaskazini mwa nchi hiyo, wenye utajiri wa gesi.

Msemaji wa Wizara ya Ulinzi ya Msumbiji, Kanali Omar Saranga, alisema katika kikao cha waandishi wa habari mjini Maputo kuwa sasa wanayadhibiti majengo ya serikali, bandari, uwanja wa ndege, hospitali na vituo vingine muhimu.

Mji wa Mocimboa da Praia ambako mashambulizi ya kwanza ya itikadi kali yalifanywa Oktoba 2017, tangu mwaka jana umetumika kama makao makuu ya wapiganaji wenye mahusiano na Kundi linalojiita Dola la Kiislamu - IS, wakijiita Al-Shabaab nchini humo.

Msemaji wa Jeshi la Pamoja Kanali Ronald Rwivanga alisema mji huo wa bandari ulikuwa ngome ya mwisho ya wanamgambo hao na kukombolewa kwake kunaashiria mwisho wa awamu ya kwanza ya operesheni za kupambana na uasi wa itikadi kali.

Wanajeshi wa Msumbiji wamekuwa wakipambana kukamata udhibiti wa mkoa wa Cabo Delgado, eneo lenye mojawapo ya miradi mikubwa zaidi ya gesi asilia, mradi wa dola bilioni 20 unaoendeshwa na kampuni kubwa ya nishati ya Total ya Ufaransa.

Rwanda ilipeleka askari 1,000 mwezi uliopita, ili kulipiga jeki jeshi la Msumbuji.

Wiki iliyopita walipata mafanikio yao ya kwanza tangu walipoingia nchini humo, wakisema walelisaidia jeshi la Msumbiji kukamata udhibiti wa Awasse, eneo dogo, lakini la kimkakati la makazi karibu na Mocimboa da Praia.

**DW**

## Hofu yatawala uchaguzi mkuu kesho kutwa Zambia

**Lusaka,** ZAMBIA

ZAMBIA iko katika hali ya sintofahamu siku chache, kabla ya uchaguzi mkuu, Agosti 12, mwaka huu.

Angalau watu watatu wameuawa katika makabiliano kati ya wafuasi.

Vurugu hizo zilisababisha kupelekwa kwa jeshi katika maeneo mbalimbali, Agosti Mosi, mwaka huu.

Wagombea 16, watapambana katika uchaguzi wa urais, wawili ndio wanapewa nafasi kubwa katika uchaguzi huo.

Rais anayemaliza muda wake Edgar Lungu wa Chama cha Patriotic Front, na Hakainde Hichilema, Chama cha United Party for National Development (UPND), ambaye anawania mara ya sita.

Edgar Lungu na Hakainde Hichilema watachuana Alhamisi, kwa mara ya tatu.

Uchunguzi uliochapishwa kuhusiana na uchaguzi huo unatoa takwimu tofauti.

Katika uchunguzi wa kwanza, Lungu anapewa ushindi kwa asilimia 44 ya kura.

Takwimu zilionekana kuwa nzuri sana kwa baadhi ya wachambuzi na ambazo zilikataliwa na uchunguzi wa pili.

Uchunguzi wa pili unampa Hichilema ushindi kwa asilimia 24.

Wengi waliohojiwa wanakataa kuonyesha ni nani watakayempigia kura, ishara ya kuongezeka kwa hofu uchaguzi huu.

Kwa wiki moja, jeshi limekuwa likifanya doria katika mitaa ya Lusaka kudumisha utulivu, baada ya vifo vya wafuasi watatu wa vyama vya kisiasa, wakiwamo wawili kutoka chama tawala.

Upinzani na waangalizi wengi, wana hofu kuwa askari watatishia wapigakura. **RFI**

## Mwandishi auawa Kivu Kaskazini

**Kinshasa,** DRC

MWANDISHI Héritier Magayane, ambaye bado kijana wa kituo cha runinga ya serikali (RTNC), ameuawa kwa kuchomwa kisu usiku wa Jumamosi, kuamkia Jumapili eneo la Rutshuru, Mkoa wa Kivu Kaskazini, Mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), eneo linalokumbwa na mgororo wa usalama.

Héritier Magayane (26), baba watoto wawili, alikuwa akifanya kazi katika kituo cha RTNC tangu mwaka 2018 huko Rutshuru, amesema mmoja wa wafanyakazi wenzake, Roger Sebyeradu.

Alipokea simu kutoka kwa mtu wake wa karibu ambaye alimuomba kukutana naye kwa mazungumzo na huko ndiko aliuawa, alisema Luc Albert Bakole Nyengeke, mkuu wa eneo la Rutshuru, ambaye ni ofisa wa jeshi.

Makundi kadhaa yenye silaha yanatekeleza vitendo vya kikatili katika jimbo hilo, eneo linalohusika linadhibitiwa na jeshi la FARDC, mauaji haya yanaweza kuwa mabaya, alisema, huku akiwataka raia kusubiri matokeo ya uchunguzi uliofunguliwa Jumapili asubuhi.

"Tunaamini kuwa mauaji yake yanahusiana na makala aliyokuwa akirusha hewani", alisema Roger Sebyeradu, "kwa sababu baada ya kumuua waliondoka na simu yake". Héritier Magayane alikuwa akirusha hewani makala yanayohusiana na vijana, akiwashauri kutunza amani kutokana na kukosekana kwa usalama katika mkoa huo.

Kivu Kaskazini na mkoa jirani wa Ituri imekuwa chini ya sheria ya kijeshi tangu mapema mwezi Mei, hatua ya kipekee iliyotangazwa na Kinshasa, kujaribu kukomesha mashambulizi na vitendo vya uhalifu vya makundi yenye silaha ambayo yanatishia raia tangu miaka ya 1990. **RFI**




Waziri Mkuu Japan, Yoshihide Suga, akiwa amebeba shada la maua eneo la Nagasaki Peace Park, kusini mwa nchi hiyo, kwa ajili ya kuweka kwenye sehemu yenye kumbukumbu ya bomu la atomiki lililopigwa eneo la Hiroshima, ikiwa ni miaka 76 tangu tukio hilo. **PICHA: AP**

## Binti wa miaka 14 afariki dunia akijifungua kanisa lisiloamini tiba

**Harare,** ZIMBABWE

POLISI Zimbabwe wanachunguza kifo cha msichana mwenye umri wa miaka 14 kilichotokea wakati anajifungua, kesi hiyo imeibua hisia mbalimbali miongoni mwa wananchi na wanaharakati wa haki za binadamu.

Memory Machaya ameripotiwa kufariki mwezi uliopita katika madhabau Mashariki mwa mji wa Marange.

Kesi hiyo imeelezewa kuwa ni unyanyasaji wa watoto, binti huyo aliripotiwa kulazimishwa kuacha shule ili aolewe.

Umoja wa Mataifa (UN), umetaka serikali kuidhinisha kuwa mimba za utotoni ni uhalifu na kusitisha utamaduni huo.

Shirika hilo limesema wasiwasi wake mkubwa na kulaani vikali ripoti kuhusu kifo cha binti huyo.

Shirika hilo lilisema linatoa maelezo juu ya wasiwasi wake mkubwa na limelaani vikali ripoti zinazoelezea jinsi kifo kilivyojitokeza.

"Hali iliyopo sasa ya kutotatua kesi za unyanyasaji kwa wanawake na wasichana nchini Zimbabwe, zikiwamo kesi za ndoa za utotoni, haiwezekani kuendelea kupuuziwa," taarifa ya UN ilieleza Jumamosi.

Kifo cha binti huyo kilichotokea Julai 15, mwaka huu, kimetoa angalizo juu ya mimba za utotoni katika kanisa la Zimbabwe Apostolic, ambalo limekuwa linakataa dawa na tiba za hospitalini.

Familia yake ilisema mtoto alipona na alijifungua salama, vyombo vya habari vya ndani vimeripoti.

Mazingira ambayo yalipelekea kifo chake kuchunguzwa na polisi na tume ya jinsia nchini humo.

Baadhi ya watu waliandika maombi yao mtandaoni kwa kutaka haki itendeke juu ya kifo cha binti huyo Memory Machaya, mpaka sasa saini za watu zaidi ya 57,000 zinataka haki ipatikane.

Mwanaharakati wa Zimbabwe wa kutetea haki za wanawake Everjoice Win alisema ni wakati muafaka kwa watu kuweka msukumo kwa walio madarakani kuweka sheria mpya.

"Wanawake na wasichana hawaonekani kama binadamu waliokamilika wenye haki ... na kuwa na mamlaka ya miili yao," aliandika kwenye Twitter.

Kisheria, wasichana wa Zimbabwe wanaruhusiwa kuolewa wakiwa na miaka 18, wakati miaka 16 kuwa na idhini ya kujamiiana.

Baadhi ya familia wanaamini kuwa ndoa za utotoni zina manufaa ya kifedha.

Mabinti wengi wanaoolewa wakiwa wadogo wana matumaini kuwa ndoa itawapatia fursa ya kwenda shule.

Hata hivyo, mabinti hao huishia kupata mimba mara tu ya kuolewa na hivyo kubaki kuwa mama wa nyumbani.

**BBC**

# RODRIGUEZ

## PSG WATATISHA WAKIMSAJILI MESSI

**LONDON, England**

JAMES Rodriguez anaamini kwamba, Paris Saint-Germain inaweza kuanza kusherehekea ushindi wa mapema katika kila mashindano huko Ufaransa kama Lionel Messi atajiunga na klabu hiyo msimu huu wa majira ya joto.

Muargentina huyo anapatikana kama mchezaji huru baada ya Alhamisi Barcelona kuthibitisha kuondoka kwake, na PSG sasa ndio wanaopewa nafasi kubwa ya kumsajili, hata hivyo ina kikwazo cha kifedha.

"Kama Messi atakwenda PSG watakuwa kwenye ligi ya kwao Ufaransa," James alisema. "Wape majina yote tayari.

"Sidhani kama mtu yeyote nchini Uingereza anaweza kulipa mshahara wake, labda Manchester City tu."

Mchezaji huyo wa Colombia aliendelea kuzungumza juu ya hali ya Messi, na akaonyesha huruma kwa Sergio Aguero.

"Kun Aguero alikwenda Barcelona na sasa Messi anaondoka," James aliongeza. "Ni marafiki".

"Lakini huo ndiyo mpira wa miguu. Vivyo hivyo vilinitokea. Nilikwenda Everton, kwa sababu Carlo Ancelotti alikuwapo na sasa angalia."




# Tuanzebe arejea tena Aston Villa

**LONDON, England**

BEKI wa Manchester United, Axel Tuanzebe amerejea Aston Villa kwa mkopo kwa mara ya pili.

Tuanzebe aliisaidia Villa kupanda Ligi Kuu katika msimu wake wa kwanza klabuni hapo 2018-19, na sasa amejiunga tena na safu ya kocha Dean Smith, kabla ya kampeni yao ya tatu mfululizo katika Ligi Kuu.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23, aliangukia nyuma ya wachezaji kama Harry Maguire, Victor Lindelof na Eric Bailly, katika kikosi kinachocheza United katika msimu uliopita, lakini sasa atakuwa na nafasi ya kucheza dakika za kawaida, pale Villa Park.

'Mashetani Wekundu' wamethibitisha kuondoka kwa Tuanzebe katika taarifa rasmi, pia wakisema kwamba beki huyo wa kati amesaini mkataba mpya, hapo Old Trafford hadi 2023.

"Axel Tuanzebe atatumia kampeni ya msimu wa 2021-22 kwa mkopo pale Aston Villa baada ya kukubali uhamisho wa msimu mzima kwa klabu hiyo ya Ligi Kuu," taarifa ya klabu hiyo kwa waandishi wa habari ilisomeka.



# SILVA, KANE KUPISHANA

**LONDON, England**


KLABU ya Manchester City ipo tayari kumtumia kiungo wao wa Kireno, Bernardo Silva kama chambo kwa ajili ya kumnasa mshambuliaji wa Tottenham, Harry Kane, ambaye anatajwa kuwa na thamani ya pauni milioni 150.

Mabingwa hao wa Ligi Kuu England, waliripotiwa kuweka mezani kitita cha pauni milioni 100, ambazo ziligomewa hivyo wanaamini kumtumia Silva kama chambo kunaweza kuwa mpango ambao pengine unaweza kuwavutia Spurs.

Kane ambaye siku chache zilizopita alizua gumzo kutokana na kutohudhuria progamu kadha za mazoezi za timu hiyo, amerejea Jumamosi na kujumuika na wenzake kwa ajili ya maandalizi ya msimu ujao wa Ligi Kuu England.

Msimu uliopita Manchester City inayonolewa na Pep Guardiola iliachana na aliyekuwa mshambuliaji wao, Sergio Aguero, hivyo mpango uliopo mbele yao ni kuhakikisha anapatikana wa kuziba pengo lake na chaguo lao, la kwanza ni Kane.

Ikumbukwe kuwa Kane ndiye aliyekuwa mfungaji bora wa Ligi Kuu England kwa msimu uliopita akiwa na mabao 23.



## HABARI MICHEZO



# MARTIAL ATAKIWA SERIE A

**MILAN, Italia**

WAKATI Inter Milan wakiwa mbioni kumwachia Romelu Lukaku, Anthony Martial anarejea tena kwenye rada za mabingwa hao watetezi wa Ligi Kuu Italia, Serie A.

Lukaku anakaribia kutua Stamford Bridge, miaka miwili baada ya kutoka Old Trafford na kwenda San Siro.

Upande wa pili, baada ya miaka miwili, Inter wanahusishwa tena na Martial kama mbadala wa Lukaku.

Chelsea na Inter wamekubaliana dau la pauni milioni 100 kwenye usajili wa Lukaku, ni suala la muda tu kabla ya mchezaji huyo kutambulishwa rasmi pale Stamford Bridge.

Anthony Martial amekuwa kwenye wakati mgumu ndani ya United na inaripotiwa kuwa, Man wameweka thamani ya pauni milioni 50 kwa timu inayomtaka mshambuliaji huyo.

Si Inter tu wanaohusishwa na Martial, ndani ya Ligi Kuu England, klabu za Tottenham Hotspurs na Everton pia zinahusishwa na mshambuliaji huyo ambaye ni dhahiri atakuwa na wakati mgumu zaidi kupambania namba.

Inter wanataka kusajili washambuliaji wawili baada ya Lukaku kuondoka.

Edin Dzeko, yupo kwenye mchakato wa kujiunga na Inter akitokea AS Roma.

# AGUERO ARITHI JEZI YA MESSI BARCA

**BARCELONA, Hispania**

KWA mujibu wa Jarida la El Larguero, mshambuliaji mpya wa Barcelona, Sergio Aguero anatarajiwa kurithi jezi namba 10 ya Lionel Messi pale Camp Nou.

Mshambuliaji huyo atakabidhiwa jezi hiyo maarufu kabla ya kampeni za msimu wa 2021-22 kuanza, hii ni kutokana na klabu hiyo kulazimishwa kuachana na mshindi wa Ballon d'Or mara sita kwa vigezo vya kanuni na masharti ya fedha za Ligi Kuu Hispania, LaLiga.

Mshambuliaji Memphis Depay, anatarajiwa kuvaa jezi namba tisa akiichukua kutoka kwa Martin Braithwaite, wakati Ansu Fati akikabidhiwa jezi namba 17.

Aguero aliyetokea Manchester City kama mchezaji huru, aliifungia klabu hiyo mabao 260 katika mashindano yote huku akitwaa mataji 12 katika miaka 10 aliyocheza EPL.




# MARTINEZ HATAKI KUONDOKA

**MILAN, Italia**

MSHAMBULIAJI wa Inter Milan, Lautaro Martínez, hana nia ya kujiunga na Tottenham Hotspur, wakala wake amedai.

Kocha mpya wa Spurs, Nuno Espirito Santo, tayari ameimarisha kikosi chake msimu huu wa majira ya joto kwa kumsajili Bryan Gil, Pierluigi Gollini na Cristian Romero.

Na Mreno huyo anasemekana anataka kumfanya mchezaji wa kimataifa wa Argentina, Martinez kuwa saini yake ya nne ya msimu huu wa majira ya joto.

Gazeti la Times linadai Spurs wamekubali dau kubwa la pauni milioni 60 kwa mshambuliaji huyo.

Lakini mwakilishi wa Martinez, Alejandro Camano, anasisitiza mteja wake hana nia ya kuondoka Milan.




Alisema: "Lautaro anafurahi huko Inter na nchini Italia. Uamuzi wake ni kukaa huko."

Camano ameongeza: "Hatakuwa na vita na Inter kuondoka klabuni. Lautaro ni mchezaji wa Inter na anafurahi nchini Italia."

Martinez amekuwa lulu kwa Inter tangu aliposaini mkataba wa miaka mitano huko San Siro Julai mwaka 2018.

Nyota huyo amefunga mabao 49 na kutoa pasi za mwisho 20 katika mechi 149 kwa Inter.

Na kwa mujibu wa Times, Tottenham ina mpango wa kumchezesha Martinez pamoja na nahodha Harry Kane, ambaye mustakabali wake klabuni hapo uko hewani.

## KWA UFUPI

### BAYERN YAMTAKA HAALAND

MKURUGENZI wa michezo wa Bayern Munich, Hasan Salihamidzic amethibitisha kuwa klabu hiyo ya Ujerumani ina nia ya kumsajili mshambuliaji wa Norway mwenye umri wa miaka 21, Erling Braut Haaland kutoka kwa wapinzani wao wa Bundesliga, Borussia Dortmund. ***(Goal)***

### UNITED YAMTAKA GRIEZMANN

MANCHESTER United wanajiandaa kutoa ombi la kupata huduma za mshambuliaji wa Ufaransa, Antoine Griezmann mwenye umri wa miaka 30. ***(Todofichajes)***

### MOURINHO AMTAKA ICARDI

KOCHA wa AS Roma, Jose Mourinho anataka sana kumsajili mshambuliaji wa Paris St-Germain, Mauro Icardi mwenye umri wa miaka 28, huku Edin Dzeko wa Bosnia, 35, akionekana kukaribia kuondoka mji mkuu wa Italia kwenda Inter Milan. ***(Gazzetta dello Sport)***

### PSG, MESSI KIMEELEWEKA

MSHAMBULIAJI wa Argentina, Lionel Messi mwenye umri wa miaka 34, jana Jumatatu alitarajiwa kufanyiwa vipimo vya afya kabla ya kukamilisha uhamisho wa bure kwenda Paris St-Germain. ***(L'Equipe)***

### ARSENAL YAMTAKA TRIPPIER

KLABU ya Arsenal iko tayari kufanya usajili wa beki wa Atletico Madrid, Kieran Trippier kwani Manchester United imeshindwa kukubaliana na ada kwa mabingwa hao wa Hispania kwa mchezaji huyo wa England mwenye umri wa miaka 30. ***(Sun)***

### BARCA KUISHTAKI PSG

BARCELONA wanajaribu kuzuia jaribio lolote la PSG kumsaini Lionel Messi kwa kufungua malalamiko kwa Tume ya Ulaya ikisema klabu hiyo ya Ufaransa itakiuka sheria za matumizi ya fedha ikiwa watafanikiwa kumsajili Muargentina huyo. ***(Marca)***

### SPURS YAJITOSA KWA MESSI

KLABU ya Tottenham Hotspur ni miongoni mwa zinazojaribu kumsajili Lionel Messi baada ya Barca kusema hatosalia Nou Camp. ***(Express)***

### WILLOCK HUYO NEWCASTLE

KLABU ya Newcastle wamekubaliana na Arsenal kuhusu ada ya zaidi ya pauni milioni 20 kumsajili kiungo, Joe Willock.

### VLAHOVIC AWANIWA ARSENAL

ARSENAL inashindana na Tottenham kuwania saini ya mshambuliaji wa Fiorentina, Dusan Vlahovic, huku Spurs ikimtaka mchezaji huyo wa miaka 21 kama mbadala wa Harry Kane, ambaye anawindwa na Manchester City. ***(Sky Sport Italia's Gianluca Di Marzio)***

### CHAMBERLAIN KWA SOUTHAMPTON

KLABU ya Southampton inajaribu kumsajili tena kiungo wa kati wa England mwenye umri wa miaka 27 wa Liverpool, Alex Oxlade-Chamberlain, miaka 10 baada ya kuondoka St Mary's. ***(Sun)***

### CARVALHO AGOMBEWA ULAYA

KLABU za Porto, West Ham, Leeds na Norwich zinahusishwa na kiungo wa kati wa Uingereza mwenye umri wa miaka 18, Fabio Carvalho. ***(Mail)***



# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# MESSI AKUBALIANA MKATABA NA PSG

●●●Familia yangu na mimi tuliamini tutakaa hapa nyumbani, wote tulitaka zaidi ya kitu chochote, lakini...

**BARCELONA, Hispania**

BAADA ya juzi mshambuliaji wa Argentina, Lionel Messi kutangaza rasmi kuondoka kwake klabu ya Barcelona baada ya kuichezea kwa takriban miaka 21, hatimaye nyota huyo mwenye umri wa miaka 34 amekubaliana mkataba wa miaka miwili na Paris St-Germain.

Gazeti la Ufaransa la L'Equipe liliripoti kuwa Messi alitarajiwa kufanyiwa vipimo vya afya yake mjini Paris Saint-Germain jana Jumatatu asubuhi.

Katika taarifa kwa vyombo vya habari Jumapili katika Uwanja wa Nou Camp, Messi aliyeshindwa kujizuia aliangua kilio wakati alipokuwa akiaga klabu hiyo.

"Familia yangu na mimi tuliamini kuwa tutakaa hapa nyumbani, ndivyo sote tulitaka zaidi ya kitu chochote.

"Tulifanya hapa kuwa nyumbani na tulifikiri tutaishi Barcelona.

"Wakati ambao nimekuwa nao hapa umekuwa mzuri usiokuwa na kifani, lakini leo lazima nisema kwaheri. Nimekuwa hapa miaka mingi sana, maisha yangu yote tangu nilipokuwa na miaka 13.

"Ningependelea kushinda taji lingine la Ligi ya Mabingwa Ulaya, naamini tungeliweza kushinda tena kwa maoni yangu," aliendelea kusema.

Pia alizungumzia uhusiano wake na Barcelona akisema: "Nilijitolea kupunguza mshahara wangu kwa asilimia 50, lakini hawakuniuliza kitu kingine chochote. Habari nilizoomba asilimia 30 zaidi ni uwongo, mambo mengi ambayo watu wanasema si kweli."

Mamia ya mashabiki wa Barcelona walikusanyika nje ya Nou Camp wakati wa mkutano wa Messi na waandishi wa habari.

Kuondoka kwa Messi si pigo tu kwa Barcelona, pia ni pigo kwa LaLiga, ambayo imepoteza mfungaji mabao wake hodari.

Messi alizaliwa na kukulia katikati mwa Argentina, kisha alihamia Hispania na kujiunga na Barcelona akiwa na umri wa miaka 13, na kuichezea klabu hiyo kwa mara ya kwanza Oktoba 17, mwaka wa 2004.

Alijiimarisha kama mchezaji muhimu wa klabu ndani ya miaka mitatu iliyofuata, na katika msimu wake wa kwanza bila kukatizwa mnamo 2008-09 alisaidia Barcelona kufanikiwa kushinda mataji matatu ya soka nchini na akiwa na umri wa miaka 22, Messi alishinda tuzo yake ya kwanza ya Ballon d'Or.

HABARI MICHEZO

# YANGA KATIKATI YA SAUZI NA MOROCCO

**Adam Fungamwango na Saada Akida**

KIKOSI cha timu ya Yanga bado kipo katikati kuamua ama kiweke kambi Afrika Kusini au kiwafuate watani zao Simba, Morocco kujiwinda na msimu ujao wa mechi za kimataifa, Ligi Kuu sambamba na michuano mingine.

Kaimu Katibu Mkuu wa klabu hiyo, Haji Mfikirwa, amesema wamekuwa na mipango ya kuiweka kambini timu hiyo nje ya nchi na wanafikiria kwenda nchini Morocco au Afrika Kusini.

"Ni sahihi tupo katika mipango hiyo, tunaangalia Morocco au Afrika Kusini. Siku hizi mbili tatu tutakamilisha mipango na tutawataarifu. Lakini hili ni sahihi tunataka kuweka kambi nje ya nchi kwa ili kupata utulivu wa kutosha kwa ajili ya maandalizi ya msimu unaokuja. Unajua tutakuwa na mashindano makubwa zaidi na hivyo tunatakiwa kujiandaa zaidi kwa sababu ukiangalia msimu uliopita hatukupata yale mazoezi mazuri ya mwanzo ya msimu na matokeo yake tumeyaona, yalituathiri," alisema Kaimu Katibu Mkuu huyo.

Alisema wachezaji wa timu hiyo wataanza rasmi mazoezi Jumapili wiki hii na wachezaji tegemeo wataanza kuonekana chini ya Kocha Mkuu, Nasreddine Nabi.

Yanga kama itakwenda Morocco kuweka kambi, itakaa nchi moja na watani zao wa jadi, Simba ambao tayari wameshatangaza dhamira yao ya kuweka kambi nchini humo.

Mwenyekiti wa Klabu hiyo, Murtaza Mangungu, alisema wanakwenda kuweka kambi nchini humo kwa ajili ya kuajiandaa na msimu mpya wa ligi.

"Tumepanga kwenda nchini Morocco. Ni nchi kubwa yenye vifaa na miundominu mizuri kwa ajili ya kambi na ni tulivu," alisema mwenyekiti huyo.

Simba imeanza mazoezi Jumapili, ambapo wachezaji wake wengi wamekusanyika kwa ajili ya maandalizi ya msimu mpya.

## Kiduku apania kutangazwa ubabe kwa Dulla Mbabe

**Na Christina Haule, Morogoro**

BONDIA Twaha Kiduku, amesema anatarajia kulipa fadhila kwa wadhamini wa pambano lake na Dulla Mbabe kwa kuhakikisha anaibuka na ushindi Agosti 20, mwaka huu, watakapopanda ulingoni jijini Dar es Salaam kuwania gari.

Akizungumzia mchezo huo jana, Kiduku aliwashukuru wadhamini wa mchezo huo kwa kuona umuhimu wa kuwashindanisha na kuahidi kutoa burudani safi kwa mashabiki wake kwa kuhakikisha anarudi na ushindi nyumbani, Morogoro.

Kwa upande wa mdhamini wa pambano hilo Promota Suleiman Semunyu, alisema maandalizi yanaendelea vizuri na kwamba wataanza na mapambano ya utangulizi kutoka kwa mabondia tofauti wa ndani ya Morogoro yatakayofanyika Jumamosi wiki hii Msamvu, Morogoro, ambapo aliwaomba wadau wa ngumi kujitokeza kupata burudani hiyo.

"Katika pambano la Kiduku na Twaha Mbabe litakaofanyika Ukumbi wa Ubungo Plaza jijini Dar es Salaam, mabondia hao watashindania gari aina ya Crown Athlete lenye thamani ya zaidi ya shilingi milioni 18," alisema Semunyu.

Kwa upande wa wadau wa mchezo wa ngumi mkoani Morogoro wakitoa maoni yao kuelekea pambano hilo, wengi walimtahadharisha Mbabe, wakimtaka kujiandaa kisaikolojia kupokea kipigo kikali siku hiyo dhidi ya mpinzani wake, Kiduku.

Wakizungumza na Nipashe kwa nyakati tofauti wadau hao akiwamo Nestory Alexander, alisema mchezo wa ngumi unahitaji nidhamu na kumsikiliza mwalimu mambo ambayo Kiduku anayaishi na ndiyo yatakayomfanya kutoka na ushindi na kurudi na gari siku hiyo.

Alexander alisema kutokana na mazoezi anayoyafanya Kiduku milimani ikichangiwa na nidhamu yake mchezoni, ana uhakika atampa kipigo Mbabe.

Mdau mwingine, Godfrey Kasambula, alisema anaamini kwa asilimia 100 kuwa Kiduku atashinda katika pambano hilo kwa kuwa ni bondia mzuri na mwenye uwezo na amekuwa akiuonyesha kwenye mapambano ya mwanzo ambapo katika pambano la kwanza walitoka sare na la pili Kiduku alishinda, hivyo nahili nalo atashinda.

TUMEREJEA...




Wachezaji wa Simba, Clatous Chama na Perfect Chikwende wakipozi katika picha baada ya kuwasili Uwanja wa Ndege wa Julius Nyerere, Dar es Salaam juzi, tayari kwa kujiunga na kikosi cha timu hiyo kujiandaa na msimu mpya wa Ligi Kuu na michuano ya kimataifa. **MPIGAPICHA WETU**

## Coastal yagundua ilipojikwaa Ligi Kuu

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa Coastal Union umesema umejifunza na hautakubali kurudia makosa yaliyojitokeza msimu ulioisha katika suala la usajili wa wachezaji wakuimarisha kikosi chao kuelekea msimu mpya wa Ligi Kuu Tanzania Bara unaotarajiwa kuanza Septemba 29, mwaka huu.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Katibu Mkuu wa timu hiyo, Rashid Mgweno, alisema msimu huu mpya wanasajili wachezaji wazuri na wenye uzoefu wa kucheza mechi za ushindani.

Alisema msimu ulioisha hawakuwa na kikosi imara kutokana na usajili walioufanya kwa kuwapa nafasi vijana lakini sasa makosa hayo hatajirudia tena kwa sababu wamejipanga kuiimarisha timu yao.

"Usajili umeshaanza kwa kamati husika kuingia vitani kufanyia kazi mapendekezo ya kocha Juma Mgunda, katika ripoti hiyo imeonyesha beki wa kati, viungo na washambuliaji.

"Tumeshaanza kufanya mazungumzo ila kwa sasa ni mapema kuwataja kwa sababu wachezaji hao nao wamekuwa wakitakiwa na timu zingine, kikubwa tumejipanga kuimarisha na kuwa na timu imara kwa msimu huu mpya," alisema Mgweno.

## Mobby ajifunga mmoja Geita Gold

**Na Saada Akida**

BEKI kisiki aliyekuwa akihusishwa na Simba, Iddy Mobby, amesaini mkataba wa mwaka mmoja kuitumikia Geita Gold FC, itakayoshiriki Ligi Kuu Tanzania Bara kwa mara ya kwanza katika msimu wa 2021/22 unaotarajiwa kuanza Septemba 29, mwaka huu.

Mobby aliwahi kuhusishwa kutakiwa na Simba kwa msimu wa 2019/20 na sasa amejiunga na Geita Gold FC akitokea katika kikosi cha Polisi Tanzania FC, iliyoachana naye msimu uliomalizika.


Wachezaji wengine waliosaini mkataba kuitumikia timu hiyo ni Daniel Lyanga (miaka miwili) akitokea Ruvu Shooting, Kelvin Naftali (mwaka mmoja) na Yusuph Kagoma (miaka miwili) akitoke Gwambina FC iliyoshuka daraja.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mwenyekiti wa Geita Gold FC, George Mbiligeda, alisema usajili wa nyota hao ni mapendekezo ya benchi la ufundi kulingana na mahitaji ya timu yao kuelekea msimu mpya wa Ligi Kuu.

"Tumeanza kusajili wachezaji wenye uzoefu ili kutoa ushindani mkubwa katika Ligi Kuu, tumefanikiwa kuwasajili nyota hao sita na tunaendelea na mchakato wa kuimarisha kikosi cha timu yetu," alisema Mbiligeda.

# Michezo

Jumanne Agosti 10, 2021
Nipashe



## Messi akubaliana mkataba na PSG

HABARI UK. 22

NIMESAINI...



Kiungo mkabaji mpya wa Yanga, Khalid Aucho (kulia), akiwa na Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Usajili pia Mkurugenzi wa Uwekezaji wa Kampuni ya GSM, wanaoidhamini klabu hiyo, Mhandisi Hersi Said, baada ya mchezaji huyo kusaini mkataba wa kuitumikia miamba hiyo ya mtaa wa Twiga na Jangwani, Dar es Salaam jana. **PICHA: YANGA**

# KISINDA APIGWA BEI, AUCHO AITULIZA YANGA

## Amfuata Ibenge Morocco kwa Sh. milioni 346, wapoozwa pia kwa ofa ya kambi huku...

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI Yanga jana ikikamilisha usajili wa kiungo mkabaji mpya wa kimataifa wa Uganda, Khalid Aucho, imepata pigo baada ya kukubali kumuuza winga wao machachari, Mkongomani Tuisila Kisinda kwenda RS Berkane ya Morocco.

Kisinda sasa anakwenda kuungana na aliyekuwa kocha wake mkuu wakati akiitumikia AS Vita ya kwao DR Congo, Florent Ibenge, ambaye alijiunga na timu hiyo ya Morocco kwa mkataba wa miaka miwili Julai 5, mwaka huu.

Akizungumza na Nipashe jana, Ofisa Habari wa Yanga, Hassan Bumbuli, alithibitisha klabu hiyo kumuuza Kisinda kwa RS Berkane kwa dola za Marekani 150,000 sawa na Sh. milioni 346.7 za Tanzania.

"Ni kweli tumemuuza Tuisila Kisinda kwa dola 150,000, na siyo kiasi hicho tu cha fedha bali pia klabu hiyo ya Morocco itagharamia kambi yetu ya kujiandaa na msimu mpya kwa muda wa siku 11 nchini humo, ikiwa ni sehemu ya makubaliano ya kuwauzia mchezaji huyo," alisema Bumbuli.

Kisinda ni mmoja wa wachezaji wapya waliosajiliwa na Yanga msimu uliopita na kuonyesha kiwango kikubwa katika kikosi hicho kwa kuisaidia kumaliza nafasi ya pili kwenye Ligi Kuu Bara na kucheza fainali ya Kombe la FA dhidi ya Simba iliyotetea taji hilo.

Ibenge ameonyesha nia ya kukijenga kikosi chake hicho, kwani mbali na Kisinda, tayari ameutaka uongozi wa klabu hiyo ya Morocco kuhakikisha inamsajili mshambuliaji wa Simba, Mkongomani Chris Mugalu, aliyemaliza msimu akiwa na mabao 15 moja nyuma ya mfungaji bora, John Bocco wanayecheza naye klabu moja.

Hata hivyo, wakati mashabiki wa Yanga jana wakichachamaa kupitia mitandaoni ya kijamii kwa kuonyesha kutofurahishwa na hatua ya klabu yao kumuuza Kisinda, kiungo mpya aliyekamilisha usajili wa kujiunga na klabu hiyo jana, Aucho, amesifu ukubwa wa klabu hiyo huku akieleza na yeye ataonyesha ukubwa wake.

"Mimi ni mchezaji mkubwa na mwenye malengo makubwa, Yanga ni timu kubwa yenye malengo makubwa. Mimi sasa ni kijani na bluu," alisema Aucho ambaye amesaini mkataba wa miaka miwili.

Nyota huyo ambaye alitua nchini usiku wa kuamkia jana, sasa ataungana na wachezaji wenzake kuingia kambini Jumapili wiki hii wakiwa chini ya Kocha Mkuu, Mmorocco Nasreddine Nabi.

Aucho amejiunga na Yanga, akiwa mchezaji huru baada ya kumaliza mkataba wake na klabu ya Misr Lel Makkasa ya Misri.

Kwa usajili huo, Aucho anakuwa mchezaji mpya wa tano Yanga kusajiliwa na kutambulishwa rasmi baada ya kipa raia wa Mali, Djigui Diarra kutoka Stade Malien ya kwao na washambuliaji Wakongo, Fiston Mayele kutoka AS Vita na Heritier Makambo kutoka Horoya ya Guinea sambamba na mzawa Yussuf Athumani kutoka Biashara United ya Mara.

Yanga ambayo bado inaendelea kufanya usajili wa nyota wapya kukijenga kikosi chake, imesema itaingia kambini Jumapili kujiandaa na Ligi Kuu Bara, Ligi ya Mabingwa Afrika pamoja na mashindano mengi kabla ya baadaye kwenda kujichimbia nje ya nchi.

# Simba SC wachanja corona, Mkude ndani

**Na Mwandishi Wetu**

WACHEZAJI wa Simba pamoja na benchi zima la ufundi, wamefika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili jana na kupata chanjo ya kujikinga na virusi vya corona, huku pia kiungo wao mkabaji kipenzi cha mashabiki wa timu hiyo, Jonas Mkude, akiwa miongoni mwao baada ya kurejeshwa kikosini.

Mkude amerejeshwa kikosini Simba baada ya kusimamishwa kwa takriban miezi miwili kwa tuhuma za utovu wa nidhamu, hatua iliyomfanya kukosa mechi nyingi za mzunguko wa pili hadi timu hiyo inatwaa ubingwa wa Ligi Kuu na Kombe la FA.

**Mkude alituhumiwa kwa makosa yanayojirudia na utoro na kuchelewa kambini na Kamati ya Nidhamu ya klabu chini ya Mwenyekiti, Kamanda Mstaafu wa Jeshi la Polisi, Suleiman Kova ikashauri akapimwe akili ili kujua tatizo linalomsumbua hadi kufanya makosa ya kujirudia.**

Simba inatarajia kuanza mazoezi rasmi leo kujiandaa na msimu mpya wa Ligi Kuu Bara, Ligi ya Mabingwa Afrika pamoja na mashindano mengine ikiwamo Kombe la FA.

Tayari Shirikisho la Soka Afrika (CAF), limetangaza kuwa michuano yake, Ligi ya Mabingwa na Kombe la Shirikisho Afrika, itaanza rasmi Septemba 10, mwaka huu ikiwa ni siku 19 kabla ya Ligi Kuu Bara kuanza.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002